**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI**




# MAFANIKIO YA MIAKA HAMSINI (50) YA UHURU KATIKA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI


MIAKA HAMSINI YA UHURU TANZANIA BARA

1961-2011

TUMETHUBUTU, TUMEWEZA TUNAZIDI KUSONGA MBELE







S.L.P 9280
DAR ES SALAAM JULAI 2011

# YALIYOMO

**DIBAJI KUTOKA KWA WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI..........6**

**MANENO YA UTANGULIZI KUTOKA KWA KATIBU MKUU..........8**

**TAARIFA MUHIMU KUHUSU JUMUIYA..........10**

**1.0 UTANGULIZI..........12**

1.1 Historia Fupi ya Ushirikiano katika Afrika Mashariki.......... 12
1.2 Kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwanzo 1967.......... 12
1.3 Madhumuni ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 1967.......... 12
1.4 Mafanikio Katika Ushirikiano wa Mwanzo Katika Afrika Mashariki.......... 13
  1.4.1 Shirika la Reli.......... 13
  1.4.2 Shirika la Posta.......... 13
  1.4.3 Shirika la Bandari.......... 14
  1.4.4 Shirika la Ndege.......... 14
  1.4.5 Benki ya Maendeleo.......... 14
1.5 Kuvunjika kwa Jumuiya ya Mwanzo ya Afrika Mashariki 1977.......... 15
1.6 Athari za Kuvunjika kwa Iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki.......... 15

**2.0 JUMUIYA MPYA YA AFRIKA MASHARIKI.......... 16**
2.1 Hatua Zilizochukuliwa Baada ya Kuvunjika kwa Jumuiya ya Mwanzo.......... 16
2.2 Kuundwa Upya kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, 1999.......... 16
2.3 Hatua Zilizochukuliwa Kuepuka Kuvunjika Tena kwa Jumuiya.......... 16
2.4 Malengo ya Jumuiya mpya.......... 17
2.5 Maeneo ya Ushirikiano.......... 18
2.6 Faida za kuanzishwa kwa Jumuiya.......... 19
  2.6.1 Faida za Kiuchumi.......... 19
  2.6.2 Faida za Kijamii.......... 19

**3.0 KUANZISHWA WIZARA YA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI...... 20**
3.1 Miundo ya Wizara na Jumuiya na Jinsi Ilivyobadilika.......... 21
  3.1.1 Muundo wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.......... 21
  3.1.2 Muundo ulivyorekebishwa tarehe 26 Januari, 2009.......... 23
  3.1.3 Muundo Ulivyorekebishwa Tarehe 26 Februari, 2010.......... 23
3.2 Muundo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.......... 25
  3.2.1 Mkutano wa Wakuu wa nchi *(Summit)*.......... 25
  3.2.2 Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki.......... 25
  3.2.3 Kamati ya Makatibu Wakuu.......... 26
  3.2.4 Kamati za Kisekta.......... 26
  3.2.5 Mahakama ya Jumuiya.......... 26
  3.2.6 Bunge la Afrika Mashariki.......... 28

3.2.7 Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ........ 29
3.3 Taratibu za Utendaji na Maamuzi ........ 32
3.3.1 Utaratibu wa Utendaji ........ 32
3.3.2 Taratibu za Maamuzi ........ 32
3.3.3 Taratibu za Uenyekiti katika Jumuiya ........ 32

**4.0 MAJUKUMU NA MALENGO YA WIZARA NA JUMUIYA ........ 32**
4.1 Majukumu na Malengo ya Wizara ........ 32
4.2 Madhumuni ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ........ 33

**5.0 HALI YA UTAWALA NA UONGOZI WA WIZARA ........ 34**
5.1 Hali ya Utawala na Uongozi katika Wizara ........ 34
5.1.1 Mawaziri ........ 34
5.1.2 Manaibu Mawaziri ........ 34
5.1.3 Makatibu Wakuu ........ 34
5.1.4 Naibu Katibu Mkuu ........ 35
5.1.5 Wakurugenzi ........ 35
5.1.6 Wakurugenzi Wasaidizi ........ 36
5.1.7 Wakuu wa Vitengo ........ 37
5.1.8 Mgawanyo wa Jinsia Katika Ngazi za Uongozi 2010/11 ........ 38
5.1.9 Idadi ya Watumishi ........ 38
5.2 Hali ya Utawala na Uongozi Katika Jumuiya ........ 39

**6.0 SERA, MIKAKATI NA SHERIA YA WIZARA ........ 41**
6.1 Sera, Mikakati na Sheria Katika Wizara ........ 41
6.2 Sera na Sheria ........ 41
6.3 Sera, Mikakati, Sheria na Itifaki Katika Jumuiya ........ 41
6.3.1 Sera na Mikakati Katika Jumuiya ........ 41
6.3.2 Sheria na Itifaki Katika Jumuiya ........ 42


**7.0 MABADILIKO NA MATUKIO MAKUU ........ 44**
7.1 Matukio Makuu katika Jumuiya ........ 44

**8.0 MAFANIKIO KATIKA MTANGAMANO WA AFRIKA MASHARIKI ........ 53**
8.1 Kuanzisha Taasisi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ........ 55
8.1.1 Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria (LVBC) ........ 55
8.1.2 Oganaizesheni ya Uvuvi Katika Ziwa29 Victoria (LVFO) ........ 55
8.1.3 Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki (IUCEA) ........ 56
8.1.4 Wakala wa Usalama wa Anga Afrika Mashariki (CASSOA) ........ 56
8.1.5 Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki (EADB) ........ 56
8.2 Mafanikio Katika Utekelezaji wa Hatua za Mtangamano ........ 56

8.2.1 Umoja wa Forodha....57
8.2.1.1 Utekelezaji wa Vipengele Muhimu vya Umoja wa Forodha.... 58
8.2.1.2 Mafanikio ya Utekelezaji wa Umoja wa Forodha.... 61
8.2.2 Utekelezaji wa Soko la Pamoja.... 63
8.2.2.1 Maeneo ya msingi katika Soko la Pamoja.... 63
8.2.3 Umoja wa Fedha....67
8.2.4 Shirikisho la Kisiasa.... 68
8.2.5 Uimarishaji wa Sekta Binafsi.... 68
8.2.6 Ushirikiano baina ya Jumuiya (EAC) na Kanda Nyingine.... 69
8.2.6.1 Utatu wa EAC-COMESA-SADC (*EAC-COMESA-SADC Tripate Arrangement*)....69
8.2.6.2 Ubia wa Kiuchumi kati ya Jumuiya ya Afrika Mashairiki n Jumuiya ya Ulaya.... 70
8.3 Mafanikio Katika Utekelezaji wa Miradi na Programu za Kikanda....70
8.3.1 Uendelezaji wa Miundombinu.... 70
8.3.2 Uendelezaji wa Barabara....71
8.3.3 Uendelezaji wa Sekta ya Reli....74
8.3.4 Uendelezaji wa Sekta ya Nishati....76
8.3.5 Sekta ya Usafiri wa Anga....78
8.3.6 Sekta ya Usafiri wa Majini....78
8.3.7 Kuanzisha Vituo vya Pamoja vya Utoaji Huduma Mipakani....78
8.3.8 Miradi ya Zanzibar.... 79
8.3.9 Uendelezaji wa Sekta ya Kilimo.... 79
8.3.10 Uendelezaji wa Miradi na Programu za Huduma za Jamii.... 80
8.3.11 Mafanikio Katika Sekta ya Siasa, Ulinzi na Usalama.... 82
8.3.12 Utekelezaji wa Mradi wa Utunzaji Mazingira ya Ziwa Victoria.... 84
8.3.13 Ujenzi wa Makao Makuu ya Jumuiya.... 85
8.3.14 Upanuzi wa Jumuiya.... 86

**9.0 CHANGAMOTO.... 86**
9.1 Changamoto Katika Ngazi ya Jumuiya.... 86
9.1.1 Uhaba wa Raslimali Fedha....86
9.1.2 Kuendelea Kuwepo kwa Vikwazo Visivyo vya Kiforodha.... 86
9.2 Changamoto za Kiundeshaji Katika Ngazi ya Wizara.... 87
9.2.1 Kuhuishwa kwa Masuala ya Mtangamano.... 87
9.2.2 Mwamko na Uelewa Mdogo Juu ya Masuala ya Mtangamano....87
9.2.3 Majukumu Kutoendana na Raslimali.... 87

**10.0 MATARAJIO KATIKA KIPINDI CHA MIAKA 50 IJAYO.... 87**



# DIBAJI

*kutoka kwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki*

Ili kujenga uelewa wa pamoja kuhusu Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, katika kusherehekea miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara, imeonelea hakuna budi jamii ya kitanzania ikafahamishwa kuhusu mafanikio na hatua mbalimbali ambazo Jumuiya ya Afrika Mashariki imefikia tangu kuvunjika kwa Jumuiya ya awali mwaka 1977, na kuanzishwa kwa Jumuiya mpya hapo mwaka 1999.

Maadhimisho ya Miaka 50 ya uhuru wa Tanzania Bara yameikuta Nchi yetu katika uchumi wa sasa unao lazimisha ushindani katika mfumo wa utandawazi uliioshamiri na wenye changamoto nyingi. Mtangamano wa kikanda ni hatua muhimu sana kuelekea katika mtangamano wa kiuchumi wa dunia/kimataifa. Kwa kipindi cha miongo miwili mpaka miaka ya 2000, Uchumi wa nchi za Afrika ulikuwa ni wa kusuasua sana kutokana na changamoto nyingi za kisera, usimamizi, na kubwa zaidi ikiwa ni uwezo wa bidhaa za nchi hizi zinazoendelea kupenya katika soko la dunia. Katika hali hii, pamoja na jitihada mahsusi zilizochukuliwa za kurekebisha sera za kiuchumi, Nchi hizi ziliona bado kuna umuhimu wa kuungana kikanda ili kujipa sauti ya pamoja katika kupambana na changamoto za uchumi wa dunia/kimataifa *(global economic integration)* na hatimaye kunufaika na fursa zinazotokana na mfumo mzima wa utandawazi. Nchi za Afrika Mashariki zilikwisha litambua hili tangu miaka ya 1960 pale wakuu wa Nchi za Kenya, Uganda na Tanzania walipoamua kuunda Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Pamoja na changamoto zilizopelekea Jumuiya ya awali kuvunjika, bado miaka ishirini baadaye viongozi wetu waliona umuhimu wa kuunganisha tena nguvu zao kwa manufaa ya watu wao. Lengo kuu likiwa ni kuanzisha ushirikano wa kikanda utakaoziunganisha Sekta za Umma na Sekta Binafsi, ili kuwawezesha Wanaafrika Mashariki kupanua fursa za kiuchumi na kijamii na kuwaletea wananchi wao maendeleo.
Hivyo, kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kulilenga kupanua na kuimarisha ushirikiano wa watu wa Afrika Mashariki ambao umedumu kwa muda mrefu hata kabla nchi hizi hazijapata uhuru. Ushirikiano huu umekusudia kuharakisha ukuaji wa uchumi na kuboresha maisha ya wananchi wake kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Jumuiya ya Afrika Mashariki ni miongoni mwa Jumuiya chache za kikanda katika dunia zinazokua na kuimarika kwa kasi na hata kuweza kupata mafanikio makubwa sana kwa kipindi cha miaka kumi tu tangu kuanzishwa kwake upya.

Chapisho hili limeandaliwa mahsusi, kwa ajili ya kuelezea mafanikio yaliyofikiwa tangu Jumuiya ya awali na mpaka sasa. Chapisho hili linatoa fursa ya kuelewa nafasi na malengo ya Tanzania kama mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, pia nafasi na umuhimu wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki katika kuhakikisha Tanzania inanufaika ipasavyo na ushirikiano huu ikiongozwa na dira na dhamira ya taifa la Tanzania, kuiwezesha Tanzania kuwa Taifa la Uchumi wa kati unaongozwa na ongezeko la mauzo nje (kikanda na kimataifa) kama ajenda yake (namba moja.)

Afrika Mashariki **tumethubutu, tumeweza, tunazidi kusonga mbele,** kila mmoja atimize wajibu wake, inawezekana!

---

**Samuel J. Sitta (Mb),**

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI**
**JUNI, 2011**

---



# MANENO YA UTANGULIZI

*kutoka kwa Katibu Mkuu, WUAM*

Serikali ya Tanzania inasherehekea miaka 50 ya Uhuru wake huku ikishuhudia mafanikio ya kimaendeleo katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Maendeleo hayo yanatokana na sera na mikakati mbalimbali ikiwemo matumizi ya ushirikiano wa kikanda kama majowapo ya nyenzo za kukuza uchumi na kujiletea maendeleo.

Ushirikiano za Afrika Mashariki una historia ndefu tangu na kabla ya Uhuru. Mwaka 1905 Uganda na Kenya zilianzisha Bodi ya Sarafu Moja ya Afrika Mashariki mwaka 1905, na iliyokuwa Tanganyika ilijiunga na Bodi hiyo mwaka 1922. Mwaka, 1917 Kenya na Uganda zilianzisha Umoja wa Forodha, na Tanganyika ilijiunga mwaka 1922. Aidha, mwaka 1948 Kamisheni ya Ushirikiano ilianzishwa. Mwaka 1961 Mashirika ya Pamoja ya Huduma *(Common Services Oraganizations)* yalianzishwa ikiwa ni pamoja na Shirika la Posta na Mawasiliano *(Post and Telecommunication)*; Shirika la Reli na Bandari *(East African Railways and Harbours)*; Shirika la Ndege la Afrika Mashariki *(East African Airways)*; Taasisi ya Usafiri wa Anga *(East African Aviation Services)*; Taasisi ya Uchunguzi ya ugonjwa wa malale; na Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki *(East African Development Bank)*.

Hatua zilizoonyeshwa hapo juu zilifuatiwa na kuimarikai zaidi kwa mtangamano wa nchi hizi tatu baada ya Tanzania kupata uhuru wake, ambapo Jumuiya ya Afrika Mashariki iliundwa mwaka 1967. Shabaha ya Jumuiya ilikuwa kuimarisha na kuongeza uhusiano uliopo baina ya Nchi Wanachama katika masuala ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na shughuli nyingine ili kuleta maendeleo ya haraka ambayo matunda yake yaligawanywa kwa usawa baina ya Nchi Wanachama.

Baada ya kuvunjika kwa Jumuiya, Nchi Wanachama zilitiliana saini Makubaliano ya Kugawana Mali na Madeni *(Mediation Agreement for the Division of Assets and Liabilities)* hapo mwaka 1984. Katika makubaliano hayo, kulikuwa na kipengele kilichotoa fursa kwa nchi hizi kutafuta maeneo ya ushirikiano na kuandaa mpango thabiti wa jinsi ya kushirikiana. Kipengele hiki kiliwawezesha Wakuu wa Nchi mnamo mwaka 1993 kusaini makubaliano ya kuanzisha Kamisheni ya Kudumu ya Utatu *(The Permanent Tripartite Commission)*. Kufuatia makubaliano haya, Ushirikiano wa Afrika Mashariki ulianza tena rasmi mwaka 1996 kwa kuanzishwa kwa Sekretarieti ya Kudumu ya Utatu wa Afrika Mashariki *(The East African Community Secretariat of the Permanent Tripartite Commission)*, iliyozinduliwa rasmi tarehe 14 Machi, 1996 katika Makao Makuu ya Jumuiya Mjini Arusha, Tanzania.

Baada ya hapo majadiliano ya kuianzisha upya Jumuiya ya Afrika Mashariki yalianza na kuwezesha kuundwa upya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Jumuiya hii ilianzishwa mwaka 1999 kwa Wakuu wa Nchi kusaini Mkataba wa Kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki tarehe 30 Novemba 1999, na kwanza kutumika rasmi tarehe 7 Julai, 2000. Kulingana na makubaliano hayo, Jumuiya ya Afrika Mashariki ni Taasisi ya Kiserikali *(inter-Governmental Organization)*, iliyoanzishwa na nchi za Tanzania, Kenya na Uganda. Nchi za Rwanda na Burundi zilijiunga katika Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 2007.

Tangu kufufuliwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Nchi Wanachama zimeendelea na utekelezaji wa hatua za mtangamano na miradi na programu za pamoja ikiwa ni kuanzisha mipango kabambe mbalimbali katika sekta mbalimbali zinazolenga kukuza uchumi wa nchi za Afrika Mashariki.

Jarida hili limelenga kutoa taarifa kuhusu Ushirikiano katika kanda ya Afrika Mashariki hususan, mafanikio yaliyopatikana katika Jumuiya ya Afrika Mashariki toka Tanzania ipate uhuru hapo tarehe 9 Desemba, 1961 hadi sasa, na matarajio ya Wizara na Tanzania kwa ujumla katika kipindi cha miaka 50 ijayo.

***TUMETHUBUTU, TUMEWEZA, NA TUNASONGA MBELE***

---

**Dkt. Stergomena L. Tax**

**KATIBU MKUU**
**WIZARA YA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI**

---

# TAARIFA MUHIMU KUHUSU JUMUIYA

**Jumuiya:**

- Inajumuisha nchi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Jamhuri za Burundi, Kenya, Rwanda, Uganda
- Ina jumla ya eneo la kilomita za mraba milioni 1.82;
- Ina idadi ya watu wanaokadiriwa kuwa milioni 133.5 (hadi Juni, 2010)
- Ina pato la ndani la Dola za Kimarekani bilioni 74.5 (hadi Mei, 2010)
- Ina wastani wa Pato la Taifa kwa kila mtu la Dola za Kimarekani 558 (Hadi Mei, 2010)

**Dira ya Jumuiya ya Afrika Mashariki:**


- Kuwa na Jumuiya iliyositawi na kuimarika kiushindani, kiusalama, na iliyoungana kisiasa.

**Dhima ya Jumuiya:**

- Kupanua na kuimarisha ushirikiano kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni ili kuboresha maisha ya watu wa Afrika ya Mashariki kwa kuongeza ushindani, thamani katika uzalishaji, biashara na uwekezaji.

## ALAMA ZA UTAMBULISHO ZA JUMUIYA ZINAJUMUISHA:

**Bendera**



**Nembo**

EAC

JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

**Maana ya Rangi za Bendera:**

Bluu ikimaanisha Ziwa Viktoria ambayo ni alama ya umoja wa Nchi Wanachama; Nyeupe, Nyeusi, Kijani, Manjano na Nyekundu zinawakilisha rangi mbalimbali za bendera za Nchi Wanachama. Mikono iliyoshikana ikimaanisha Umoja wa Jumuiya na alama ya katikati ni Nembo ya Jumuiya.

**Kauli mbiu ya Jumuiya:**

Watu wamoja lengo moja. Huu ni wito wa umoja na ukumbusho wa dira ya Jumuiya
ya Afrika Mashariki.

**Lugha ya Jumuiya:**

Lugha rasmi ya Jumuiya ni Kiingereza, na Kiswahili ni lugha ya mawasiliano.

**Vigezo vya kujiunga: Nchi / Muombaji anatakiwa:-**

- Kuikubali Jumuiya kama ilivyoainishwa katika Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya
- Kuzingatia misingi ya utawala bora, demokrasia, utawala wa sheria, kuheshimu haki za binadamu na haki za kiraia
- Kuwa na mchango mkubwa katika kuimarisha mtangamano ndani ya eneo la Afrika Mashariki
- Iwe na nafasi kijiografia kupakana na nchi mojawapo mwanachama
- Iwe yenye kujenga na kuendeleza uchumi wa soko; na
- Iwe yenye sera za kiuchumi na kijamii zinazowiana na zile za Jumuiya
- Mkutano wa Wakuu wa Nchi Wanachama ndiyo wenye maamuzi ya kuiruhusu nchi kujiunga na Jumuiya

## WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

**Jumuiya Yetu sote tuilinde; Tuwajibike tuimarike; Umoja wetu ni nguzo yetu; Idumu Jumuiya yetu.**

1. *Ee Mungu twakuomba uilinde*
*Jumuiya Afrika Mashariki*
*Tuwezeshe kuishi kwa amani*
*Tutimize na malengo yetu.*

2. *Uzalendo pia mshikamano*
*Viwe misingi wa Umoja wetu*
*Natulinde Uhuru na Amani*
*Mila zetu na desturi zetu.*

3. *Viwandani na hata mashambani*
*Tufanye kazi sote kwa makini*
*Tujitoe kwa hali na mali*
*Tuijenge Jumuiya bora.*

na simu ya nchi tatu iliunganishwa na kuwa Shilika la Posta na Simu la Afrika Mashariki. Ulipofika mwaka 1969 Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki lilikuwa likiendesha Posta 970 na Vituo vya Simu 350 kote Afrika Mashariki.

### 1.4.3 Shirika la Bandari

Shirika la Bandari lilihusika na uangalizi pamoja na uendeshaji wa bandari zote zilizo pwani ya Afrika Mashariki.

### 1.4.4 Shirika la Ndege

Shirika la Ndege la Afrika Mashariki liliundwa mwaka 1946 likiwa ni shirika kati ya Nchi za Kenya, Uganda na Tanganyika. Mpaka kufikia mwaka 1970 shirika lilikuwa na ndege zilizokuwa zikifanya safari hadi Uingereza, Pakistan, India, Aden na Rhodesia.

### 1.4.5 Benki ya Maendeleo

Jumuiya ilianzisha Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki mwaka 1967. Katika Mkataba wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki zilibuniwa njia kadhaa ambazo zingetumiwa kuleta maendeleo katika ujengaji wa viwanda. Njia mojawapo ilikuwa ni kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Afrika Maashariki, Makao Makuu ya benki hiyo yalikuwa Kampala,Uganda. Benki hii ilipata mafanikio kadhaa ikiwa ni pamoja na:-

a.) Iliweza kutoa misaada ya kifedha na kiufundi ili kuwezesha maendeleo ya viwanda na kuendesha kazi ambazo matokeo yake ni kuleta ushirikiano baina ya nchi tatu za Afrika Mashariki.

b.) Ilisaidia nchi zile ambazo maendeleo yake ya viwanda yalikuwa nyuma kwa kuzipa misaaada zaidi ya fedha na kushirikiana na mashirika na makampuni ya maendeleo katika nchi zote tatu ili kutimiza malengo ambayo mashirika hayo hayakufanikisha bila msaada wa kifedha.

c.) Benki hiyo iliweza kuongeza ajira kwa wannchi wa Afrika Mashariki kwa kuajiri wafanyakazi katika nyanja mabalimbali.

Menejimenti ya mashirika haya ilikuwa chini ya Bodi za Wakurugenzi ambazo ziliteuliwa na Wakuu wa Nchi za Afrika Mashariki. Shughuli za mashirika yote ziliendeshwa kwa misingi ya kibiashara ili kuhakikisha kwamba gharama zote za uendeshaji zinatokana na faida inayopatikana katika uendeshaji. Kila mwaka mashirika haya yalitakiwa kutoa taarifa ya kazi zake mbele ya Baraza la Kutunga Sheria la Afrika Mashariki.

### 1.5 Kuvunjika kwa Jumuiya ya Mwanzo ya Afrika Mashariki 1977

Kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwanzo hapo mwaka 1977 kulitokana na sababu za kisiasa, kijamii na kimaslahi. Sababu hizo ni pamoja na:-

a.) Itikadi tofauti za kisiasa zilizokuwa zikifuatwa na Nchi Wanachama;
b.) Kutoelewana katika mgao wa mapato kutoka katika mashirika ya huduma za pamoja na kutokuwepo kwa Sera ya kushughulikia tatizo hilo;
c.) Athari za vita baridi baina ya Amerika na Urusi kwa wakati huo;
d.) Ushiriki mdogo wa sekta binafsi na vyama vya kiraia katika uendeshaji wa Jumuiya;
e.) Mtizamo finyu kuhusu mtangamano kwa baadhi ya viongozi na watendaji; na
f.) Msukumo toka nje ya Jumuiya.

### 1.6 Athari za Kuvunjika kwa Iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki

Kuvunjika kwa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki hapo mwaka 1977 kulipelekea athari kubwa ikiwa ni pamoja na kurudi nyuma maendeleo na mafanikio yaliyotokana na mashirika ya iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki yaliyoanishwa hapo juu. Athari hizo zilikuwa ni pamoja na:

a.) Kukosekana kwa ajira.
b.) Kupotea na kukosekana kwa huduma za pamoja.
c.) Kusitishwa kwa uhuru wa watu wa Afrika Mashariki kutembea ndani ya Jumuiya, soko huru la bidhaa na huduma ndani ya Jumuiya.
d.) Kuibuka kwa mtazamo hasi wa utaifa.
e.) Kuibuka kwa ushindani usio na tija.
f.) Kuibuka kwa hujuma za kisiasa baina ya Nchi Wanachama kulikosababisha kuondoa utulivu wa kisiasa.
g.) Kutokuaminiana baina ya Nchi Wanachama.

## 2.0 JUMUIYA MPYA YA AFRIKA MASHARIKI

### 2.1 Hatua Zilizochukuliwa Baada ya Kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki

Baada ya kuvunjika kwa Jumuiya, Nchi Wanachama zilitiliana saini Makubaliano ya Kugawana Mali na Madeni *(Mediation Agreement for the Division of Assets and Liabilities)* hapo mwaka 1984. Katika makubaliano hayo, kulikuwa na kipengele kilichotoa nafasi ya nchi hizi kutafuta maeneo ya ushirikiano na kuandaa mpango thabiti wa jinsi ya kushirikiana. Kipengele hiki kilitoa fursa kwa Wakuu wa Nchi kusaini Makubaliano ya Kuanzishwa kwa Kamisheni ya Kudumu ya Utatu *(The Permanent Tripartite Commission)* iliyoanzishwa mwaka 1993. Kufuatia makubaliano haya, ushirikiano wa Afrika Mashariki ulianza tena rasmi mwaka 1996 kwa kuanzishwa Sekretarieti ya Kudumu ya Utatu *(The East African Community Secretariat of the Permanent Tripartite Commission)*. Aidha Sekretarieti ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilizinduliwa rasmi tarehe 14 Machi, 1996 katika Makao Makuu ya Jumuiya Mjini Arusha, Tanzania.

Baada ya hapo Majadiliano ya kuianzisha upya Jumuiya ya Afrika Mashariki yalianza mwaka 1999 na kuwezesha kuundwa upya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

### 2.2 Kuundwa Upya kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, 1999

Jumuiya mpya ya Afrika Mashariki ilianzishwa rasmi mwaka 1999 kwa Wakuu wa Nchi kusaini Mkataba wa Kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki tarehe 30 Novemba, 1999. Tarehe 7 Julai, 2000 Jumuiya ya Afrika Mashariki ilianza rasmi kwa kuzinduliwa na Wakuu wa Nchi (tarehe 15 Januari, 2001).

Jumuiya ya Afrika Mashariki ni Taasisi ya Kiserikali (inter-Governmental Organization), iliyoanzishwa na nchi za Tanzania, Kenya na Uganda. Nchi za Rwanda na Burundi zilijiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 2007.

### 2.3 Hatua Zilizochukuliwa Kuepuka Kuvunjika Tena kwa Jumuiya

Kutokana na uzoefu uliopatikana kufuatia kuvunjika kwa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mkataba wa Kuanzisha upya Jumuiya ya Afrika Mashariki uliandaliwa kwa kujifunza kutokana na sababu zilizopelekea Jumuiya ya awali kuvunjika. Kama njia za kuwezesha Jumuiya ya sasa isivunjike tena, Mkataba umezingatia masuala yafuatayo:

a.) Uendelezaji wa mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki hatua kwa hatua. Hatua ya Kwanza ikiwa ni Umoja wa Forodha, ikifuatiwa na Soko la Pamoja, kisha Umoja wa Fedha na hatimaye Shirikisho la Kisiasa.

b.) Kupunguza madaraka ya kimaamuzi.
c.) Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuongozwa na Wananchi wa Afrika Mashariki, na kuchochewa na Sekta binafsi ndani ya Jumuiya.
d.) Ushirikishwaji wa Asasi za Kiraia kwenye mtangamano.
e.) Kuainishwa kwa ufasaha taratibu za kujiondoa uanachama.
f.) Mtangamano imara utatokana na uchumi imara na endelevu

## 2.4 Malengo ya Jumuiya mpya

Lengo la kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kuendeleza ujirani mwema, kupanua na kuimarisha ushirikiano wa watu wa Afrika Mashariki ili kuharakisha ukuaji wa kiuchumi na kuboresha maisha ya wananchi wa Afrika Mashariki kiuchumi, kisiasa, na kijamii. Ili kufikia malengo haya, Nchi Wanachama hukubaliana kukusanya nguvu kwa pamoja kutekeleza Miradi na Programu mbalimbali za kikanda ili kufikia malengo mahususi yafuatayo:

a.) Kuhakikisha kunakuwa na ukuaji na maendeleo endelevu kutokana na uendelezaji na uwiniashaji sawia wa maendeleo baina ya Nchi Wanachama.
b.) Kuhakikisha kunakuwa na uwiano sawa wa maendeleo ya kiuchumi unaoweza kuinua hali ya maisha ya jamii.
c.) Kuimarisha matumizi endelevu ya maliasili na utunzaji wa mazingira.
d.) Kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi, kijamii na kisiasa uliojengeka kwa muda mrefu ili kujenga Jumuiya ya watu wa Afrika Mashariki.



*Wakuu wa Nchi Wakisaini Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, 30 Novemba, 1999.*


d.) Kitengo cha Ununuzi;
e.) Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano; na
f.) Kitengo cha Usimamizi wa Mifumo ya Kompyuta

Tarehe 26 Februari, 2010 Muundo ulirekebishwa na kupandisha hadhi Idara ya Utawala na Rasilimali Watu kwa kuongezewa nafasi za Wakurugenzi Wasaidizi mbili, katika sehemu ya Utawala na sehemu ya Rasilimali watu. Aidha, Idara ya Sera na Mipango iliongezewa nafasi tatu za Wakurugenzi Wasaidizi katika sehemu ya Sera na Mipango, Bajeti na sehemu ya Ufuatiliaji na Tathmini. Aidha Kitengo cha Usimamizi wa Mifumo ya Kompyuta kilibadilishwa jina kuwa Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.



**Mheshimiwa Andrew Chenge (Mb.),**

*Waziri wa Kwanza wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.*



**Bw. Omar S.M Bendera,**

*Katibu Mkuu wa Kwanza wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.*

Jedwali hapo chini linaonyesha mabaliko ya Muundo katika vipindi mbalimbali:

### 3.1.2 Muundo ulivyorekebishwa 26 Januari, 2009 - Idara tano (5) na Vitengo sita (6)

| S/N | IDARA | S/N | KITENGO |
|---|---|---|---|
| 1 | Biashara, Uwekezaji na Sekta za Uzalishaji | 1 | Uhasibu na Fedha |
| 2 | Miundombinu ya Kiuchumi na Huduma za Kijamii | 2 | Habari, Elimu na Mawasliano |
| 3 | Siasa, Ulinzi na Usalama | 3 | Ukaguzi Hesabu wa Ndani |
| 4 | Utawala na Rasilimali Watu | 4 | Ununuzi na Ugavi |
| 5 | Sera na Mipango | 5 | Usimamizi wa Mifumo ya Kompyuta |
| | | 6 | Sheria |

### 3.1.3 Muundo ulivyorekebishwa 26 Februari 2010 -Idara tano (5) na Vitengo sita (6)

| S/N | IDARA | S/N | KITENGO |
|---|---|---|---|
| 1 | Miundombinu ya Kiuchumi na Huduma za Kijamii | 1 | Uhasibu na Fedha |
| 2 | Biashara, uwekezaji na Sekta za Uzalishaji | 2 | Habari, Elimu na Mawasliano |
| 3 | Siasa, Ulinzi na Usalama | 3 | Ukaguzi Hesabu wa Ndani |
| 4 | Utawala na Rasilimali Watu | 4 | Ununuzi na Ugavi |
| 5 | Sera na Mipango | 5 | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| | | 6 | Sheria |

# THE APPROVED ORGANISATION STRUCTURE OF THE MINISTRY OF EAST AFRICAN CO-OPERATION

## (Approved by the President in June, 2011)

**MINISTER**

**PERMANENT SECRETARY**

**FINANCE AND ACCOUNTS UNIT**
CHIEF ACCOUNTANT

**ADMINISTRATION AND HUMAN RESOURCES MANAGEMENT DIVISION**
DIRECTOR

**INTERNAL AUDIT UNIT**
CHIEF INTERNAL AUDITOR

**POLICY AND PLANNING DIVISION**
DIRECTOR

**INFORMATION AND COMMUNICATION TECHNOLOGY UNIT**
PRINCIPAL COMPUTER SYSTEMS ANALYST

**PROCUREMENT MANAGEMENT UNIT**
PRINCIPAL SUPPLIES OFFICER

**LEGAL SERVICES UNIT**
PRINCIPAL LEGAL OFFICER

**GOVERNMENT COMMUNICATION UNIT**
PRINCIPAL INFORMATION OFFICER

**ECONOMIC INFRASTRUCTURE AND SOCIAL SUPPORT SERVICES DIVISION**
DIRECTOR
- ECONOMIC INFRASTRUCTURE SECTION
- SOCIAL AND SUPPORTIVE SERVICES SECTION

**POLITICAL, DEFENCE AND SECURITY AFFAIRS DIVISION**
DIRECTOR
- POLITICAL AFFAIRS SECTION
- DEFENCE AND SECURITY AFFAIRS SECTION

**TRADE, INVESTMENT AND PRODUCTIVE SECTORS DIVISION**
DIRECTOR
- TRADE, FINANCE AND INVESTMENT SECTION
- PRODUCTIVE SECTORS SECTION

### 3.2 Muundo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki

Ibara ya 9 ya Mkataba wa kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki imeainisha Vyombo *(Organs)* na Taasisi zinazounda Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Vyombo *(Organs)* na Taasisi za Jumuiya ni kama ifuatavyo:

a.) Mkutano wa Wakuu wa Nchi *(Summit);*
b.) Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki;
c.) Kamati ya Makatibu Wakuu;
d.) Kamati za Kisekta;
e.) Mahakama ya Jumuiya;
f.) Bunge la Afrika Mashariki; na
g.) Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

#### 3.2.1 Mkutano wa Wakuu wa Nchi *(Summit)*

Ibara ya 12 ya Mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki imeainisha kuwa Mkutano wa Wakuu wa Nchi *(Summit)* utaundwa na Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mkutano huu unaongozwa na Mwenyekiti ambaye huchaguliwa miongoni mwa Wakuu wa Nchi kwa utaratibu wa mzunguko kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja. Mkutano wa Kilele hufanyika angalau mara moja kwa mwaka. Maamuzi ya Mkutano wa Kilele hufanyika kwa utaratibu wa maridhiano *(consensus)*. Mkutano wa Kilele ndio chombo kikuu cha maamuzi kinachotoa dira na mwelekeo wa jumla katika kutekeleza na kufikia malengo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

#### 3.2.2 Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki

Kulingana na Ibara ya 13 ya Mkataba, Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki linaundwa na Mawaziri wenye dhamana ya masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kutoka Nchi Wanachama na Mawaziri wengine kutoka sekta mbalimbali kama Nchi Mwanachama itakavyoona inafaa. Ibara ya 14 ya Mkataba imeainisha majukumu ya Baraza la Mawaziri. Pamoja na mambo mengine, Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki lina jukumu la kufanya maamuzi ya kisera, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Miradi na Programu za Jumuiya kulingana na Mkataba unaounda Jumuiya ya Afrika Mashariki. Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki ni chombo kikuu cha kuwashauri Wakuu wa Nchi. Aidha, Baraza hili pia ni chombo kikuu cha kusimamia uendelezaji wa Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na utekelezaji wa maamuzi ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi. Baraza la Mawaziri hukutana angalau mara mbili kwa mwaka.

Baraza la Mawaziri limepewa uwezo wa kuunda Mabaraza ya Mawaziri wa Kisekta kushughulikia masuala yanayojitokeza katika kutekeleza Mkataba wa Kuanzishwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hivyo, Baraza la Mawaziri la Afrika Mashariki hukasimu madaraka yake kwa Mabaraza ya Kisekta na hivyo Maamuzi ya Mabaraza hayo ni sawa na maamuzi ya Baraza la Mawaziri la Afrika Mashariki, isipokuwa kwa masuala ya kisera na yanayohitaji rasilimali.

### 3.2.3 Kamati ya Makatibu Wakuu

Ibara ya 17 ya Mkataba inaainisha kuwepo kwa Kamati ya Makatibu Wakuu kama washauri wa Baraza la Mawaziri. Kamati ya Makatibu Wakuu huundwa na Makatibu Wakuu kutoka Wizara zinazoshughulikia masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Makatibu Wakuu wengine kama itakavyoamuliwa na Nchi Mwanachama. Kamati hii hukutana angalau mara mbili kwa mwaka kabla ya Mkutano wa Baraza la Mawaziri. Aidha, Makatibu Wakuu wanaweza kukutana kadri itakavyohitajika kulingana na taratibu watakazojiwekea kujadili masuala ya uendelezaji wa mtangamano, au kushughulikia masuala ya dharura kwa ombi la Mwenyekiti wa Makatibu Wakuu.


Ibara ya 18 ya Mkataba imeainisha majukumu ya Kamati ya Makatibu Wakuu ambayo ni pamoja na kutekeleza na kusimamia utekelezaji wa maamuzi ya Baraza la Mawaziri, na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji, na kutoa mapendekezo kwa Baraza la Mawaziri kuhusu uendelezaji wa Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

### 3.2.4 Kamati za Kisekta

Kamati za Kisekta zinaundwa na Baraza la Mawaziri kutokana na maombi yaliyowasilishwa na Kamati ya Makatibu Wakuu kama watakavyoona inafaa katika kutekeleza Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kamati hizi zinatambulika katika muundo wa Jumuiya kama ilivyoonyeshwa katika Ibara ya 20 ya Mkataba. Kamati za Kisekta zina jukumu la kuandaa mipango endelevu na kuainisha vipaumbele vya utekelezaji katika Sekta husika. Aidha, ni jukumu la Kamati za Kisekta kuhakikisha kwamba zinatoa taarifa za utekelezaji wa mipango yote na kuishauri Kamati ya Makatibu Wakuu njia bora za kutekeleza mipango hiyo.

### 3.2.5 Mahakama ya Jumuiya

Kulingana na Ibara ya 23 ya Mkataba, jukumu kuu la Mahakama ya Afrika Mashariki ni kuhakikisha kuwa Mkataba wa Jumuiya unazingatiwa na kutoa tafsiri sahihi ya Mkataba pale inapohitajika. Mahakama hii imegawanyika katika vitengo viwili; Mahakama ya Awali *(Court of First Instance)* na Mahakama ya Rufaa *(Appellate Court)*. Mahakama hii kwa sasa inaundwa na majaji kumi. Majaji watano wapo katika Kitengo cha Awali na watano wengine wapo katika Mahakama ya Rufaa ya Mahakama hiyo. Majaji wa Mahakama hii hupendekezwa kutoka Nchi Wanachama na kuteuliwa na Mkutano wa Kilele wa Wakuu wa Nchi kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 24 ya Mkataba. Majaji walioteuliwa hutumikia nafasi zao kwa kipindi kisichozidi miaka saba (7).



*Majaji wa Mahakama ya Afrika Mashsriki wakiwa katika moja ya majukumu yao ya kusikiliza kesi mbalimbali. Kutoka kushoto ni Waheshimiwa Majaji Kassanga Mulwa, Joseph Mulenga, Moijo ole Keiwua, na Augustino Ramadhan.*



*Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wakiwa katika picha ya pamoja siku ya uzinduzi wa Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki tarehe 30 Novemba, 2001 katika uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Mjini Arusha. Kutoka kushoto waliokaa katikati ni Waheshimiwa Marais, Benjamin William Mkapa wa Tanzania, Daniel Arap Moi wa Kenya na Yoweri Kaguta Museveni wa Uganda.*

### 3.2.6 Bunge la Afrika Mashariki

Kwa mujibu wa Ibara ya 49 ya Mkataba wa Uanzishaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Bunge la Afrika Mashariki ni chombo cha Jumuiya ambacho majukumu yake makuu ni pamoja na; kutunga sheria za Jumuiya; na kujadili na kupitisha Bajeti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki huchaguliwa na Mabunge ya Nchi Wanachama. Kila Bunge la Nchi Mwanachama huteua Wabunge tisa (9) wanaowakilisha Vyama vya Siasa vyenye uwakilishi ndani ya Bunge kwa kuzingatia jinsia na makundi mengine maalum kwa utaratibu utakaoamuliwa na Bunge la Nchi Mwanachama.

Wabunge waliochaguliwa hutumikia Bunge kwa kipindi cha miaka mitano (5) na wanaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitano. Spika wa Bunge hili huchaguliwa kutoka miongoni mwa Wabunge wa Afrika Mashariki kwa utaratibu wa mzunguko na hutumikia kipindi cha miaka mitano.



*Mheshimiwa Abdulrahman Kinana, Spika wa Kwanza wa Bunge la Afrika Mashariki.*

### 3.2.7 Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki

Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ndio chombo cha utendaji wa shughuli za kila siku za Jumuiya na kinaongozwa na Katibu Mkuu wa Jumuiya. Kazi kubwa ya Sekretarieti ni kutekeleza maamuzi ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi, Baraza la Mawaziri, Mkutano wa Makatibu Wakuu na Kamati za Kisekta kwa kushirikiana na Nchi Wanachama na Wadau wengine.

Majukumu ya Sekretarieti yameainishwa kwa kina katika Ibara ya 71 ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Majukumu haya ni kama ni kama ifuatavyo:

a.) Kuanzisha, kupokea na kuwasilisha mapendekezo katika Baraza la Mawaziri, na kuwasilisha Miswada katika Bunge la Afrika Mashariki kupitia Kamati ya Makatibu Wakuu *(Co-ordination Committee)*;

b.) Kuanzisha chambuzi na tafiti zinazohusiana

na utekelezaji wa programu kwa muda muafaka na kwa umakini ili kuhakikisha malengo ya Jumuiya yanatimia;

c.) Kupanga mikakati na kufuatilia utekelezaji wa programu kwa maendeleo ya Jumuiya;

d.) Kufanya uchunguzi na kukusanya taarifa, au kuhakiki masuala yanayoweza kuiathiri Jumuiya;

e.) Kuratibu na kuhuisha Sera na Mikakati inayohusu Jumuiya kupitia Kamati ya Makatibu Wakuu;

f.) Kuhamasisha na kutoa taarifa za Jumuiya kwa Wadau mbalimbali, Umma, na Jumuiya ya Kimataifa;

g.) Kuwasilisha ripoti za shughuli mbalimbali za Jumuiya kwa Baraza la Mawaziri kupitia Kamati ya Makatibu Wakuu;

h.) Kushughulikia shughuli za kiutawala na Menejimenti ya fedha za Jumuiya;

i.) Kutafuta fedha kutoka kwa Wahisani wa Maendeleo na vyanzo vingine kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ya Jumuiya;

j.) Kuwasilisha Bajeti ya Jumuiya kwa Baraza la Mawaziri kama inavyoelekezwa katika Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya *(Treaty)*;

k.) Kutoa mapendekezo ya ajenda za mikutano ya Vyombo vya Jumuiya isipokuwa za Mahakama na Bunge;

l.) Kutekeleza Maamuzi ya Wakuu wa Nchi *(Summit)* na ya Baraza la Mawaziri;

m.) ipasavyo mali za Jumuiya;

o.) Kutengeneza mazingira na mahusiano mazuri ya utendaji kazi na Mahakama na Bunge; na


p.) Kutekeleza masuala mengine ambayo yamebainishwa katika Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya.



*Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wakiwa katika picha ya pamoja siku ya uzinduzi wa Bunge la Afrika Mashariki uliofanyika tarehe 30 Novemba, 2001 katika uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Mjini Arusha, Tanzania. Kutoka kushoto wa pili ni Yoweri Kaguta Museveni wa Uganda, Daniel Arap Moi wa Kenya, Benjamini William Mkapa wa Tanzania, na Spika wa kwanza wa Bunge la Afrika Mashariki Mheshimiwa Ablahaman Kinana.*

MAFANIKIO YA MIAKA HAMSINI YA UHURU *KATIKA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI*

**Muundo wa Jumuiya kwa kutumia mchoro ni kama inavyoonyeshwa hapa chini:**



**IDARA: MIUNDOMBINU YA KIUCHUMI NA HUDUMA ZA KIJAMII**



**Bw. Eliabi Chodota**


**Kaimu Mkurugenzi**
27/11/2007 - 21/10/2009



**Bw.George E. Lauwo**

**Mkurugenzi**
22/10/2009 - Hadi sasa (Juni, 2011)

**IDARA: SIASA, ULINZI NA USALAMA**



**Bw. Stephen P. Mbundi**

**Kaimu Mkurugenzi**
25/2/2008 - 5/3/2009

**Kaimu Mkurugenzi**
20/7/2010 - Hadi sasa (Juni, 2011)



**Bw. Job D. Masima**

**Mkurugenzi**
6/3/2009 - 20/7/2010

## 5.1.6 Wakurugenzi Wasaidizi

Tangu wizara ianze mwaka 2006 hadi mwaka 2011 imekuwa na Wakurugenzi Wasaidizi wafuatao:

**IDARA: BIASHARA, UWEKEZAJI NA SEKTA ZA UZALISHAJI**



**Dkt. Abdullah H.**

**Makame Mkurugenzi Msaidizi, Sehemu ya Sekta za Uzalishaji**

13/10/2009 - Hadi sasa (Juni, 2011)



**Bw. Bernard Haule**

**Mkurugenzi Msaidizi, Sehemu Biashara, Uwekezaji**

13/10/2009 - Hadi sasa (Juni, 2011)


**IDARA: MIUNDOMBINU YA KIUCHUMI NA HUDUMA ZA KIJAMII**



**Bw. Eliabi Chodota**

**Mkurugenzi Msaidizi, Sehemu ya Miundombinu ya Kiuchumi**

14/8/2009 - Hadi sasa (Juni, 2011)



**Bw. Abdillah M.**

**Mataka Mkurugenzi Msaidizi, Sehemu ya Miundombinu ya Kiuchumi**

10/11/2009 - Hadi sasa (Juni, 2011)

**IDARA:ULINZI, SIASA NA USALAMA**



**Bw. Aman Mwatonoka**

**Mkurugenzi Msaidizi, Sehemu ya Masuala ya Siasa**

13/10/2009 - Hadi sasa (Juni, 2011)



**Bw. Stephen P.Mbundi**

**Mkurugenzi Msaidizi, Sehemu ya Ulinzi na Usalama**

15/5/2011 - Hadi sasa (Juni, 2011)

## 5.1.7 Wakuu wa Vitengo

Tangu wizara ianze mwaka 2006 hadi mwaka 2011 imekuwa na Wakuu Wa Vitengo wafuatao:

**IDARA: UHASIBU NA FEDHA**



**Bw. Marcel Cosmas**

**Kaimu Mhasibu Mkuu**
3/5/2006 - 30/4/2007

**Mhasibu Mkuu**
15/9/2006 - 19/4/2009



**Bibi Neema Lemunge**

**Kaimu Mhasibu Mkuu**
20/4/2009 - Hadi sasa (Juni, 2010)



**Bw Ahadi Msangi**

**Mhasibu Mkuu**
Juni 2010 - Hadi sasa (Juni, 2011)

**IDARA: HABARI, ELIMU NA MAWASILIANO**



**Flora P. Bilauri Kaimu**


**Mkuu Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano**
26/3/2008 - 2/4/2009 (Juni, 2011)



**Othman M. Othman**

**Kaimu Mkuu Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano**
12/6/2009 - 30/3/2010 (Juni, 2011)

**IDARA: TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO**



**Vedastina Justinian**

**Kaimu Mkuu Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano**
1/4/2010 - 27/7/2010

**Mkuu wa Kitengo**
27/7/2010 - Hadi sasa (Juni, 2011)


**IDARA: UKAGUZI HESABU WA NDANI**



**Richard Francis Ngoda**

**Kaimu Mkaguzi Mkuu wa Ndani**
8/2/2006 - 17/9/2006

**Mkaguzi Mkuu wa Ndani**
18/9/2006 - 18/6/2008



**Bibi Teresia Mihayo**

**Kaimu Mkaguzi Mkuu wa Ndani**
19/6/2008 - Sept 2009



**Bw. Celestin Nyaluchi**

**Kaimu Mkaguzi Mkuu wa Ndani**
-

**Mkaguzi Mkuu wa Ndani**
1/11/2010 - Hadi sasa (Juni 2011)

**IDARA: UNUNUZI NA UGAVI**



**Bw. Fredy M. G.Issa**

**Kaimu Mkuu Kitengo cha Manunuzi na Ugavi**



**Bibi Asina Kisinzah**

**Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi**
- 14/3/2011

**Mkuu Kitengo cha Ununuzi na Ugavi**


15/3/2011 - Hadi sasa (Juni 2011)

**IDARA: TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO**



**Bw. Erasto Raphael**

**Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano**



**Bibi Achentalika Mahunda**

**Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano**

Julai, 2009 - Hadi sasa (Juni 2011)

**IDARA: SHERIA**



**Bw. Mugisha Kyamani**

**Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria na Mawasiliano**
Februari 2006 - 14/3/2011

**Mkuu wa Kitengo cha Sheria**

15/3/2011 - Hadi sasa (Juni, 2011)

Mkakati wa Tatu wa Maendeleo wa mwaka 2006-2010 ulihusu utekelezaji wa maeneo ya msingi ya kisekta katika kupambana na umaskini. Sekta zilizopewa kipaumbele ni kilimo na uhakika wa chakula; viwanda; utalii na wanyamapori; miundombinu; afya; elimu; nishati; mawasiliano; utamaduni na lugha; mazingira na maliasili; na sheria na Mambo ya Mahakama. Uteuzi wa sekta hizi ulinzingatia haja ya kuleta maendeleo yaliyo sawa baina ya Nchi Wanachama, na pia kukuza uchumi na kupunguza umaskini na hivyo kuboresha maisha ya watu walio wengi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, Mkakati huu ulizingatia kuwepo kwa uwiano kati ya mipango na programu za kikanda na kitaifa.

Mkakati wa Nne wa mwaka 2011-2015 unakusudia kusaidia mipango ya ndani ya maendeleo ya Nchi Wanachama ambayo nchi moja moja zisingeweza kutekeleza au utekelezaji wake ungechukua muda mrefu kutokana na ufinyu wa Bajeti. Kwa hiyo, Mkakati huu unakusudia kuziwesha Nchi Wanachama kuweka nguvu zao pamoja na hivyo kufanikisha malengo ya msingi ya maendeleo ya kuichumi na kijamii kwa haraka zaidi.

### 6.3.2 Sheria na Itifaki Katika Jumuiya

Tangu kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1999, Nchi Wanachama zimefanikiwa kuhuisha sera na sheria kadhaa na kukamilisha Itifaki mbalimbali. Katika kipindi cha kuanzia mwaka 1999 hadi Disemba, 2010 Itifaki zilizopitishwa ni pamoja na:

a.) Itifaki ya kuanzisha Umoja wa Forodho wa Afrika Mashariki;
b.) Itifaki ya Kuzuia Usafirishaji na Usambazaji wa Madawa ya Kulevya katika Jumuiya ya Afrika Mashariki;
c.) Itifaki ya Uhakiki wa Ubora, Vipimo na Uthibiti katika Jumuiya ya Afrika Mashariki;
d.) Itifaki ya Kuanzisha Baraza la Vyuo Vikuu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki;
e.) Itifaki ya Maendeleo Endelevu katika Bonde la Ziwa Victoria;
f.) Itifaki ya kuanzisha Ushuru wa Forodha katika Jumuiya ya Afrika Mashariki;
g.) Itifaki ya Mazingira na Maliasili katika Jumuiya ya Afrika Mashariki;
h.) Itifaki ya Kuanzisha Kamisheni ya Sayansi na Teknolojia ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;
i.) Itifaki ya Kuanzisha Wakala wa Kusimamia Usalama wa Anga katika Jumuiya ya Afrika Mashariki;
j.) Itifaki ya Kuanzisha Kamisheni ya Utafiti wa Magonjwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki;
k.) Itifaki ya Kuanzisha Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;

l.) Itifaki ya Soko la Pamoja ya Afrika Mashariki; na
m.) Itifaki ya Uratibu wa Sera ya Nje ya Afrika Mashariki;

Aidha, Nchi Wanachama zimekamilisha majadiliano ya Miswada mbalimbali inayohusu masuala ya Jumuiya. Miswada hiyo kupitishwa na Bunge la Afrika Mashariki na hatimaye kuidhinishwa na Wakuu wa Nchi ili kuwa Sheria za Jumuiya. Katika kipindi cha kuanzia mwaka 1999 sheria zilizopitishwa ni pamoja na:

a.) Sheria ya Tafsiri ya Sheria za Jumuiya ya Afrika Mashariki *(The East African Community Interpretation Act)*;
b.) Sheria ya Nembo ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki *(The East African Community Emblem Act)*;
c.) Sheria ya Mamlaka na Kinga kwa Wabunge wa Afrika Mashariki *(The East African Legislative Assembly Powers and Privileges Act)*;
d.) Sheria ya Kutunga Sheria za Jumuiya *(The Acts of the Community Act)*;
e.) Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki *(The East African Community Customs Management Act 2004)*;
f.) Sheria ya Kusimamia Usafiri katika Ziwa Victoria *(The Lake Victoria Transport Management Act 2007)*;
g.) Sheria ya Wakuu wa Nchi kutoa Mamlaka kwa Vyombo vingine vya Jumuiya *(The Summit – Delegation of Powers and Functions Act 2007)*;
h.) Sheria ya Mapato na Matumizi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 2002, 2003, 2004, 2005, 2006, 2007,2009 na 2009;
i.) Sheria ya Uhakiki wa Ubora, Vipimo na Udhibiti katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, 2006;
j.) Sheria ya Ushindani ya Afrika Mashariki, 2006;
k.) Marekebisho ya Sheria ya Kutunga Sheria za Jumuiya ya Afrika Mashariki, 2008;
l.) Sheria ya Baraza la Vyuo Vikuu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, 2008;
m.) Marekebisho ya Sheria ya Nembo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, 2008; na
n.) Marekebisho ya sheria ya Kusimamia Ushuru wa Forodha katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, 2008.


# 7.0 MABADILIKO NA MATUKIO MAKUU

## 7.1 Matukio Makuu katika Jumuiya

Mabadiliko na matukio makuu kuhusiana na mtangamano wa Afrika ya mashariki tangu Tanzania ipate uhuru ni kama ifuatavyo:

### 1967:


Jumuiya ya Afrika Mashariki yaundwa na hivyo kuashiria mwanzo wa kutumia kwa azma ya Marehemu Mwalimu Julius Kambarage ya kuunda muungano wa Afrika Mashariki;



*Kutoka kushoto ni Waheshimiwa Marais Hayati Milton Obote wa Uganda, Hayati Jomo Kenyatta wa Kenya na Hayati Julius Nyerere wa Tanzania.*

### 1977:

Iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki yavunjika na kusababisa mtikisiko mkubwa wa kiuchumi katika Afrika Mashariki na hususan, katika Nchi zilizotegemea huduma kadhaa za kikanda katika kuendesha uchumi wake. Huduma zilizoathirika sana zilihusu uchukuzi na usafirishaji (nchi kavu, majini na angani), mawasiliano (simu na posta).



*Moja ya ndege za lililokuwa Shirika la Ndege la Afrika Mashariki.*

**1991:**

Viongozi wa Nchi za Afrika Mashariki, walipokutana katika mkutano wa Wakuu wa Jumuiya ya Madola uliofanyika Harare, Zimbabwe ambapo Viongozi hao walikubalina kuanzisha tena ushirikiano wa Afrika Mashariki.



*Kutoka kushoto ni Waheshimiwa Marais Daniel Arap Moi wa Kenya, Ali Hassan Mwinyi wa Tanzania na Yoweri Kaguta Museveni wa Uganda na Viongozi wengine wa Serikali.*

**30 Novemba, 1993:**

Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika Mashariki walitia Sahihi ya kuanzishwa kwa Tume ya Kudumu Utatu ya Ushikiano wa Afrika Mashariki.

**Machi, 1996:**


Katibu Mkuu wa Kwanza wa Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Balozi Francis Mathaura kutoka nchi ya Kenya ateuliwa.



*Katibu Mkuu wa kwanza wa Jumuiya, Mheshimiwa Balozi Francis Mathaura kutoka Kenya.*




*Wakuu wa Nchi wakisaini Itifaki ya Soko la Pamoja jijini Arusha. Mstari wa mbele kutoka kushoto ni Rais Museveni, Rais Kagame, Rais Kikwete, Rais Kibaki na Rais Nkurunziza.*



*Katibu Mkuu wa Wizara, Dkt. Stergomena L. Tax akipokea cheti cha ungozi mahiri katika majadiliano ya Itifaki ya Soko la Pamoja, katika ngazi ya Makatibu Wakuu.*



*Naibu Katibu Mkuu wa Wizara, Bw. Uledi Abbas Mussa akipokea cheti cha ungozi mahiri katika majadiliano ya Itifaki ya Soko la Pamoja, katika ngazi ya Wataalaam.*



*Rais Paul Kagame wa Rwanda akimkabidhi uenyekeiti wa Jumuiya Rais Dkt. Jakaya Kiwkete wa Tanzania.*

**20 Novemba, 2009:**
Wakuu wa Nchi Wanachama waweka jiwe la msingi wa ujenzi wa Makao Makuu ya Jumuiya jijini Arusha.



**26 Januari, 2010:**
Wizara yazindua Mkataba wa Huduma Bora kwa wateja ili kuimarisha huduma kwa wananchama.



*Mhe. Dkt. Diodorus B. Kamala Waziri wa Ushirikiano wa Afika Mashariki akizindua Mkataba wa huduma kwa wateja, kushoto kwake ni Mhe Aboud Mohamed Aboud, Naibu wa Waziri wa Ushirikiano wa Afika Masharikì, na kulia kwake ni Dkt. Stergomena L. Tax*

**26 Janurai, 2010:**

Wizara yazindua rasmi tovuti yake, www.meac.go.tz



*Mhe. Dkt. Diodorus B. Kamala Waziri wa Ushirikiano wa Afika Mashariki akizindua Tovuti wa Wizara ya wa Ushirikiano wa Afika Mashariki*

**Januari, 2011:**

Majadiliano ya Umoja wa Fedha yaanza, ambayo ni hatua ya tatu ya mtangamano wa Afrika Mashariki.

## 8.0 MAFANIKIO KATIKA MTANGAMANO WA AFRIKA MASHARIKI

Kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1967 na kuianzisha upya Jumuiya iliyovunjika mwaka 1977 ni miongoni mwa mafanikio ya Miaka Hamsini ya Uhuru. Miongoni mwa Mafanikio makubwa yaliyopatikana hadi sasa ni kujenga moyo wa kuaminiana ambao umeongeza nguvu kwa Nchi Wanachama katika kuendeleza mtangamano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nchi Wanachama zimeongeza moyo wa ushirikiano na kuimarisha Jumuiya na kukubaliana kuendeleza mtangamano hatua kwa hatua, kwa kuanza na hatua zinazojenga misingi ya kiuchumi na kijamii (hususani Umoja wa Forodha na Soko la Pamoja) ili kuwawezesha wananchi kunufaika na ushirikiano katika Jumuiya kwa kuendeleza biashara, shughuli za kiuchumi na uzalishaji, uwekezaji na ajira na hivyo kujiongezea kipato.Hatua hizo za mwanzo zitawawezesha wananchi kuelewa na kuyashuhudia mafanikio na faida za mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na hatimaye kufikia hatua ya kuwa na Shirikisho la Kisiasa.

Mafanikio yaliyopatikana kwa ujumla ni kama yafuatayo:

**Mafanikio ya Kiuchumi**

a.) Kuanzishwa kwa Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki. na hivyo kuongeza biashara, uwekezaji na ajira miongoni mwa Nchi Wanachama;
b.) Kuanzishwa kwa Soko la Pamoja;
c.) Kupunguza vikwazo vya kibiashara katika nchi;
d.) Kutekeleza uondoaji wa ushuru wa forodha;
e.) Kuwianisha viwango vya ubora wa bidhaa zilizozalishwa katika Afrika Mashariki;
f.) Utambuzi wa vyeti vya afya vinavyotolewa na Bodi za Kitaifa kwa bidhaa zinazouzwa katika Afrika Mashariki;
g.) Utekelezaji wa mkakati wa kuendeleza uratibu wa uwezo wa utafiti wa kisayansi katika Afrika Mashariki;
h.) Kuanzishwa kwa Kamisheni ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika Mashariki (East African Community Science and Technology Commission - EASTEC);
i.) Kuanzishwa kwa Wakala wa Usalama wa Anga wa Afrika Mashariki (Civil Aviation Safety and Security Oversight Agency - CASSOA);
j.) Kuanzishwa kwa Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki (East African Kiswahili Commssion - EAKC);
k.) Kuanzishwa kwa Kamisheni ya Utafiti wa Afya ya Afrika Mashariki (East African Health Research Commission EAHRC);
l.) Kukua kwa uhuru wa soko la hisa na uendelezaji wa soko mitaji
m.) Uhuru wa soko la mitaji;
n.) Uwianishaji wa shughuli za Wizara za Fedha na Benki Kuu wakati wa maandalizi ya kusomwa kwa Bajeti;

o.) Kuwa na Wimbo wa Jumuiya;
p.) Kuanzisha programu na miradi ya pamoja ya kuendeleza miundombinu ya kiuchumi (Barabara, reli, nishati, udsafiri wa anga);
q.) Kuimarisha uwezo wa kujadiliana Katika masuala ya uchumi na biashara kwa pamoja; na
r.) Kuwepo kwa utaratibu unaowezesha kubadilisha fedha za Nchi Wanachama.

**Mafanikio Kisiasa na Kijamii**

a.) Kusainiwa kwa Mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1999;
b.) Kuridhia Itifaki mbalimbali;
c.) Kusaini Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano katika masuala ya ulinzi mwaka 2000;
d.) Kuendelea kurahisisha uhuru wa watu na bidhaa kuvuka mipaka ya nchi;
e.) Utekelezaji wa siku saba za ziada kwa magari binafsi kuvuka mipaka ya Nchi Wanachama;
f.) Kuanza kutumika kwa Hati ya Kusafiria ya Afrika Mashariki;
g.) Kuanzisha Dirisha la Afrika Mashariki kwenye viwanja vya ndege;
h.) Kutolewa kwa hati za muda za kusafiria kwa wananchi wa Afrika Mashariki;
i.) Kuwianisha fomu za uhamiaji katika vituo vya mipakani;
j.) Kuhuisha Baraza la Vyuo Vikuu la Afrika Mashariki;
k.) Kuondoa visa za wanafunzi wa Afrika Mashariki;
l.) Kuwianisha ada za vyuo vikuu;
m.) Utekelezaji wa program za kuelimisha na kuhamasisha;
n.) Utekelezaji wa program ya kubadilishana wanafunzi na wahadhiri katika ngazi ya Vyuo Vikuu;
o.) Utekelezaji wa Programu ya kudhibiti kuenea kwa magonjwa mipakani (EAIDSnet);
p.) Kuwepo kwa jukwaa la kila mwaka kuhusu masuala ya afya ya Afrika Mashariki;
q.) Kuhuisha masuala ya jinsia katika miradi na program za Jumuiya ya Afrika Mashariki;
r.) Kuwianisha taratibu za kutoa vibali vya kufanya kazi;
s.) Kuanzishwa kwa jukwaa la Wakuu wa Polisi, Wakurugenzi wa Upelelezi, Wakuu wa Operesheni, Wakuu wa Usalama kuratibu masuala ya amani na usalama ikiwemo ukaguzi na ufuatiliaji wa pamoja, kudhibiti uhalifu kupeana taarifa za uhalifu na kutekeleza Itifaki ya Kupambana na Usafirishaji Madawa Haramu ya kulevya;
t.) Kuwa na Mkakati wa Maendeleo ya sekta binafsi;
u.) Kuendesha maonyesho ya kila mwaka ya Juakali/Nguvu Kazi;
v.) Kudhibiti hali ya ukosefu wa usalama katika Ziwa Viktoria;

w.) Kudhibiti kusambaa kwa silaha ndogo ndogo haramu na nyepesi;
x.) Kuendesha mashindano ya Insha kwa wanafunzi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;
y.) Kuandaa Mkakati wa Kupambana na Majanga na Tahadhari wa Afrika Mashariki; na
z.) Kuendesha mazoezi ya pamoja ya kijeshi, utamaduni na michezo.

### 8.1 Kuanzisha Taasisi za Jumuiya ya Afrika Mashariki *(Institutions of the Community)*

Tangu Jumuiya ianishwe hapo 1999 hadi sasa imeweza kuunda Taasisi zinazosimamia utendaji katika maeneo mbalimbali ya mtangamano kulingana na sheria zinazoanzisha Taasisi hizo. Pamoja na majukumu mengine, taasisi hizi zina jukumu la kuibua na kutekeleza miradi na programu mbalimbali. Taasisi hizo ni:

a.) Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria *(Lake Victoria Basin Commission - LVBC)*;
b.) Oganaizesheni ya Uvuvi Katika Ziwa Victoria *(Lake Victoria Fisheries Organisation - LVFO)*;
c.) Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki *(Inter-University Council for East Africa - IUCEA)*;
d.) Wakala wa Usalama wa Anga ya Afrika Mashariki *(Civil Aviation Safety and Security Ovesight Agency - CASSOA)*; na
e.) Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki *(East African Development Bank - EADB)*.

Maelezo mafupi kwa kila taasisi ni kama ifuatavyo hapo chini. Aidha, maelezo ya kina kuhusu shughuli zinazofanywa na Taasisi hizi yametolewa katika Itifaki na sheria zinazoanzisha Taasisi hizi.

#### 8.1.1 Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria (LVBC)

Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria (LVBC) ni Taasisi maalum ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yenye dhamana ya kuratibu na kusimamia maendeleo endelevu ya Bonde la Ziwa Victoria. Taasisi hii inaongozwa kulingana na Itifaki ya Kuanzishwa Taasisi iliyotiwa saini tarehe 29 Novemba, 2003 na kuridhiwa mwaka 2004. Mkuu wa Taasisi hii ni Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria ambaye huajiriwa kwa vigezo vya ushindani na Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa utaratibu wa Mzunguko wa miaka mitano (5).

#### 8.1.2 Oganaizesheni ya Uvuvi Katika Ziwa Victoria (LVFO)

Oganaizesheni ya Uvuvi Katika Ziwa Victoria (LVFO) ni Taasisi ya Kikanda chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yenye Jukumu la kuratibu na kusimamia rasilimali za uvuvi katika Ziwa Victoria. Taasisi hii ilianzishwa kwa mujibu wa Makubaliano (Convention) yaliyosainiwa na Nchi Tatu waanzilishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1994. Lengo la Taasisi hii ni kukuza ushirikiano kati ya Nchi Wanachama kwa kuwianisha juhudi za kitaifa, kuendeleza hatua za uhifadhi

na taratibu za usimamizi katika kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali hai za Ziwa Victoria.

**8.1.3 Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki (IUCEA)**

Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki (IUCEA) ni Taasisi ya Kikanda iliyoanzishwa mwaka 1980 na Nchi tatu waanzilishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika kuimarisha zaidi Taasisi hii Nchi Wanachama ziliunda Itifaki iliyosainiwa na kuridhiwa na Nchi Wanachama mwaka 2002. Lengo la kuanzishwa kwa Baraza la Vyuo Vikuu ni kuwezesha mawasiliano baina ya Vyuo Vikuu ndani ya Jumuiya, na kutoa nafasi ya majadiliano yenye lengo la kuboresha masuala ya taaluma ya elimu ya juu.

**8.1.4 Wakala wa Usalama wa Anga Afrika Mashariki (CASSOA)**

Wakala wa Usalama wa Anga ya Afrika Mashariki (CASSOA) ni Taasisi ya Kikanda yenye jukumu la kusimamia usalama wa usafiri wa Anga katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Chombo hiki kilianzishwa mwaka 2007 na kuongozwa na sheria ya kuanzisha chombo hiki. Makao Makuu ya CASSOA yapo mjini Entebbe, Uganda.

**8.1.5 Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki (EADB)**

Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki (EADB) ni Taasisi kongwe iliyoanzishwa mwaka 1967 na iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kufuatia kuvunjika kwa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977. Benki hiyo ilijiunda upya na kujiendesha kwa kufuata kanuni na taratibu zake. Kwa sasa Benki hii inamilikiwa na Nchi nne Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki za Tanzania, Kenya, Uganda na Rwanda. Aidha, baadhi ya wamiliki wengine wa Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki ni pamoja na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Maendeleo la Uholanzi (FMO), Shirika la Uwekezaji na Maendeleo la Ujerumani (DEG), na Benki ya Biashara ya Afrika (CBA).

Aidha, Taasisi zifuatazo zimeidhinishwa na Baraza la Mawaziri wa Jumuiya na mchakato wa kuanzisha Taasisi hizi unaendelea:

a.) Kamisheni ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika Mashariki *(East African Science and Technology Commission- EASTECO)*;
b.) Kamisheni ya Utafiti wa Afya ya Afrika Mashariki *(East African Health Research Commission-EAHRC)*;
c.) Kamisheni ya Kiswahili; na
d.) Kamisheni ya Afya ya Afrika Mashariki.

**8.2 Mafanikio Katika Utekelezaji wa Hatua za Mtangamano**

Ibara ya 2 (1) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, imeainisha kuwa Nchi Wanachama zitaanzisha Umoja wa Forodha na Soko la Pamoja kama hatua ya mwanzo ya mtangamano. Aidha, Ibara ya 5(2) ya Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki imeainisha hatua za mtangamano wa Jumuiya kuwa ni Umoja wa Forodha, ukifuatiwa na Soko la Pamoja, kisha Sarafu

Moja, na hatimaye Shirikisho la Kisiasa. Hatua hizi hutekelezwa hatua kwa hatua zikiongozwa na utayari Nchi Wanachama, na ukamilishwaji wa hatua za awali.

**Hatua za Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki**




### 8.2.1 Umoja wa Forodha

Utekelezaji wa Umoja wa Forodha ambayo ni hatua ya kwanza ya mtangamano wa Afrika Mashariki ni miongoni mwa mafanikio ya Tanzania katika miaka hamsini ya Uhuru. Katika utekelezaji wa hatua hii, Itifaki ya Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ilisainiwa mwaka 2004 na utekelezaji wake kuanza tarehe 1 Januari 2005.

Malengo makuu ya kuunda Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki yameainishwa katika Ibara ya 3 ya Itifaki ya Umoja wa Forodha. Malengo hayo ni:

a.) Kukuza biashara;
b.) Kuongeza ufanisi katika uzalishaji;
c.) Kukuza uwekezaji wa ndani baina ya Nchi Wanachama; na
d.) Kuendeleza viwanda.

Katika kufikia malengo haya, Ibara ya 2(4-5) ya Itifaki ya Umoja wa Forodha inaainisha vipengele muhimu katika Umoja wa Forodha. Vipengele hivyo ni kama ifuatavyo:

a.) Kuondoleana Ushuru wa Forodha Katika Biashara ya Bidhaa Miongoni mwa Nchi Wanachama *(Internal Tariff Elimination)*;
b.) Kuweka Wigo wa Pamoja wa Ushuru wa Forodha kwa Bidhaa Zinazotoka Nje ya Jumuiya *(Common External Tariff)*;
c.) Kuondoa Vikwazo Visivyo vya Kiforodha *(Elimination of Non Tariff Barriers)*;
d.) Kuwa na Vigezo vya Afrika Mashariki vya Kutambua Uasili wa Bidhaa *(EAC Rules of Origin)*; na
e.) Kuwa na Sheria Moja ya Usimamizi wa Forodha Ndani ya Afrika Mashariki *(EAC Customs Management Act, 2004)*.

Aidha kila Nchi imeunda Kamati ya Kitaifa ya kushughulikia uondoaji wa vikwazo hivi. Vilevile, Jumuiya imeunda Kamati ya kikanda ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kushughulikia uondoaji wa vikwazo hivyo. Nchi Wanachama zimepiga hatua katika uondoaji wa vikwazo visivyo vya kiforodha, hasa kwa kuweka muundo wa kimfumo wa kutambua na kushughulikia vikwazo.

**D: Vigezo vya Kutambua Uasili wa Bidhaa**

Ibara ya 14 ya Itifaki ya Umoja wa Forodha inazitaka bidhaa ambazo hazitalipiwa Ushuru wa Forodha kukidhi vigezo vya Utambuzi wa Uasili wa Bidhaa wa Afrika Mashariki kama ilivyoainishwa katika Kiambatanisho cha Tatu cha Itifaki cha Uasili wa Bidhaa. Ibara ya 4(1) ya Kiambatanisho cha Uasili wa Bidhaa *(Rules of Origin)* kimeainisha vigezo vinne ili bidhaa ikubalike kuwa ina uasili wa Afrika Mashariki. Vigezo hivyo ni:

a.) Bidhaa zilizozalishwa ndani ya Nchi Mwanachama kwa asilimia 100%;
b.) Bidhaa zilizozalishwa ndani ya Nchi Mwanachama kwa kutumia malighafi toka ndani ya Jumuiya kwa kiwango kisichopungua 40%;
c.) Kiwango cha ongezeko la thamani ya uzalishaji kisichopungua 35%; na
d.) Bidhaa ambazo zimebadilika katika usindikaji *(tarrif heading)* ukilinganisha na bidhaa hizo zilipokuwa zinaingia ndani ya Jumuiya kama ilivyoonyeshwa katika jedwali la pili la uasili wa bidhaa.

Ili bidhaa iweze kunufaika na punguzo la ushuru wa forodha cheti cha uasili wa bidhaa huhitajika kama uthibitisho wa kufikia vigezo vilivyokubaliwa vya uasili wa bidhaa. Vyeti hivi hutolewa na Idara za forodha kwa upande wa nchi nne za Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi. **Kwa upande wa Tanzania vyeti hivi hutolewa na TCCIA.**

Aidha, Nchi Wanachama zimeandaa vyeti rahisi vya uasili wa bidhaa *(simplified certificates of origin)* kwa biashara ndogo ndogo zisizozidi thamani ya kiasi cha Dola za Kimarekani 500. Ili Wafanyabiashara wadogo wasilipe ushuru wa forodha kwa bidhaa zisizozidi kiasi hicho na hivyo kunufaika na fursa za soko huru la bidhaa, wanapaswa kujaza vyeti hivi katika ofisi za TRA mpakani kabla ya kuvuka mpaka. Vyeti hivi rahisi vya uasili hupatikana katika kila ofisi za TRA zilizopo mipakani bila malipo yoyote.

**E: Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Afrika Mashariki *(EAC Customs Management Act 2004)***

Tangu mwaka 2005 Mamlaka za usimamizi wa forodha za Nchi Wanachama zimekuwa zikiendesha shughuli za kiforodha katika nchi zao kwa kutumia Sheria moja ya Usimamizi wa Forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004. Aidha sheria hiyo imekuwa ikifanyiwa marekebisho na maboresho kulingana na mahitaji.

Faida ya kuwa na sheria moja ya usimamizi wa forodha ni kutoa fursa sawa kwa wafanyabiashara katika kufuata taratibu za kuagiza, kuuza nje bidhaa na ukadiriaji wa viwango vya ushuru kwa bidhaa zote toka ndani na nje ya Jumuiya.

## 8.2.1.2 Mafanikio ya Utekelezaji wa Umoja wa Forodha

### A: Uondoaji wa Ushuru wa Forodha

Nchi Wanachama zimeweza kutekeleza ratiba ya uondoaji wa ushuru wa forodha kama ilivyokubaliwa. Kuanzia Januari 2010 bidhaa zote zinazokidhi vigezo vya uasili wa bidhaa wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kupewa cheti cha uasili wa bidhaa hazitozwi ushuru wa forodha zinapouzwa ndani ya Jumuiya.

### B: Kuongezeka kwa Biashara

Kuanzishwa kwa Umoja wa Forodha kumeongeza uhai katika sekta za biashara, uwekezaji na ajira katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mwitikio chanya wa Umoja wa Forodha umepelekea utekelezaji wa Umoja wa Forodha wenye mafanikio makubwa katika kuendeleza biashara miongoni mwa Nchi Wanachama. Mauzo ya bidhaa za Tanzania katika soko la Afrika Mashariki yameendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka. Mauzo ya Tanzania katika soko la Jumuiya yaliongezeka kutoka Dola za Kimarekani Milioni 96.4 mwaka 2005 hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 117.7 mwaka 2006, sawa na ongezeko la asilimia 22.1, na kuongezeka tena hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 173.1 mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilimia 47.1. Mwaka 2008 mauzo yaliongezeka na kufikia Dola za Kimarekani milioni 315.5, sawa na ongezeko la asilimia 82.2. Katika mwaka 2009, mauzo yalipungua na kufikia dola za kimarekani milioni 263.80. Kushuka kwa mauzo ya Tanzania katika Jumuiya mwaka 2009 kulitokana na mtikisiko wa uchumi ulioikumba dunia, na mabadiliko ya tabia nchi yalisababisha ukame na mafuriko. Mauzo yalipungua kwa asilimia 16.44. Hata hivyo mwaka 2010 mauzo yaliongezeka tena kutoka Dola za Kimarekani Milioni 263.80 mwaka 2009 hadi Dola za Kimarekani Milioni 450.10 mwaka 2010 sawa na ongezeko la asilimia 70.62. **(Kiambatanisho Na.1).**

Bidhaa ambazo Tanzania inauza kwa wingi katika nchi za Afrika Mashariki ni pamoja na chumvi, vifaa vya umeme, mafuta ya kupikia, nafaka, magunia, sabuni, vifaa vya plastiki,nyama, chuma, nondo na kahawa iliyosindikwa.

### C: Kuongezeka kwa Uwekezaji

Utekelezaji wa Umoja wa Forodha unalenga pia kutoa fursa za kuongeza uwekezaji na hivyo ajira kwa watanzania. Miradi iliyowekezwa hapa nchini kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 2005 ilikuwa 35 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 39.65. Katika mwaka 2006 kulikuweko na ongezeko la miradi 38 yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 41.06 ambapo mwaka 2007 miradi mipya ilikuwa ni 27 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 50.88. Mwaka 2008 uwekezaji uliongezeka kwa miradi mipya 77 yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 310.35 na uliongezeka tena kwa miradi mipya 42 yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 83.77 katika mwaka 2009. Katika mwaka 2010 kulikuwa na miradi mipya 33 yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni

73.66. Sekta zilizoongoza katika uwekezaji ni pamoja na Uzalishaji, Ujenzi, Kilimo, Usafirishaji na Utalii **(Kiambatanisho Na. 4)**.

**D: Kuongezeka kwa Ajira**

Ongezeko la uwekezaji kutoka katika Nchi Wanachama kulifuatiwa na ongezeko la ajira mpya ambapo mwaka 2006 kulikuwa na ajira mpya 2,643, mwaka 2006 zilikuwa 5,379, mwaka 2007 zilikuwa 2,605, na mwaka 2008 zilikuwa ni 1,424 na ajira mpya mwaka 2009 zilikuwa 1,515 na katika mwaka 2010 ajira ziliongezeka hadi kufikia 4,328. Sekta zilizoongoza katika kuongeza nafasi za ajira ni pamoja na uzalishaji, ujenzi, kilimo, usafirishaji, na utalii.

**E: Kuwianisha Viwango vya Ubora**

Ili kujenga mazingira yaliyo sawa na kuondoa vikwazo visivyo vya kiforodha, Nchi Wanachama zimeandaa Sheria ya Ubora na Viwango ya mwaka 2006. Sheria hii imewianisha taratibu za ukaguzi, viwango, vifaa vya upimaji na ugezi baina ya Nchi Wanachama ili kuwezesha watumiaji wa sheria hii kutekeleza mfumo unaofanana. Idadi ya bidhaa ambazo viwango vyake vimewianishwa hadi sasa kutokana na sheria hii ni 1500. Hatua hii inaziwezesha pia Nchi Wanachama kuondoa uwezekano wa kutumia viwango kama kikwazo cha kiufundi katika biashaara *(Technical Barriers to Trade- TBT)*.

**F: Uondoaji wa Vikwazo Visivyo vya Kiforodha**

Eneo jingine ambalo Nchi Wanachama zimeendelea kushirikiana katika Umoja wa Forodha na kupata mafanikio ni Uondoaji wa Vikwazo Visivyo vya Kiforodha. Nchi Wanachama zimekubaliana programu maalum ya kuondoa vikwazo visivyo vya kiforodha katika biashara ya bidhaa. Ili kusimamia programu hii, kila Nchi imeunda kamati ya kitaifa ya kusimamia uondoaji wa vikwazo visivyo vya kiforodha *(Elimination of Non-Tariff Barriers)*. Kamati hizi ni muhimu sana katika kutatua matatizo yatokanayo na Vikwazo Visivyokuwa vya Kiforodha.

Kwa upande wa Tanzania fomu maalum zimeandaliwa zinazowezesha kubaini vikwazo katika shughuli za kibiashara. Fomu hizo zinapatikana Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, TCCIA, CTI, TRA na katika vituo vya Forodha vya mipakani. Aidha, wananchi wanaweza kupata fomu hizo katika Tovuti ya Wizara ya Afrika Mashariki. Baada ya kuzijaza wanatakiwa kuziwasilisha Wizarani moja kwa moja au kwa kutumia Tovuti yetu, yaani **www.meac.go.tz** na pia kwa njia ya posta.

Kuwapo kwa chombo hiki kumewawezesha wafanyabiashara na wasafirishaji mizigo nchini kuwasilisha kero wanazokabiliana nazo katika kufanya shughuli zao za kibiashara. Kero zilizowasilishwa zimefuatiliwa, zimejadiliwa na kupatiwa ufumbuzi. Kero hizo ni pamoja na malalamiko ya Ms. Konyagi Tanzania Ltd aliyenyimwa haki ya kupeleka konyagi nchini Kenya, na Kenya kutumia *Certificates of Origin* za COMESA badala ya zile za Jumuiya ya Afrika Mashariki; unga wa ngano unaozalishwa na Kampuni ya Mikoani Traders Ltd (Azania) kukataliwa kuingia nchini Rwanda na

Kenya kwa madai kwamba haukidhi vigezo vya uasili wa bidhaa; tofauti za sheria ya viwango vya uzito wa mizigo inayobebwa na malori *(axle load weights)* katika ya Nchi nyingine za Jumuiya na Kenya ambapo Kenya inaruhusu uzito wa juu mwisho tani 48 wakati nchi nyingine ikiwemo Tanzania zinaruhusu uzito hadi kufikia tani 56; Nchi ya Kenya kutoza ushuru wa asilimia mbili (2) kwa bidhaa za maua na mimea kinyume na makubaliano ya Umoja wa Forodha; kukataliwa kuingia nchini Kenya kwa maziwa yanayozalishwa na Kampuni ya Musoma Dairy Ltd; kukataliwa kuingia nchini Kenya kwa nyama ya ng'ombe inayozalishwa na Kampuni ya SAAFI Ltd.

### 8.2.2. Utekelezaji wa Soko la Pamoja

Uanzishwaji wa Soko la Pamoja katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ni miongoni mwa mafaniko ya miaka hamishi ya Uhuru katika sekta ya Mtangamano wa kikanda.Nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki zimeanza rasmi kutekeleza makubaliano ya kuanzisha Soko la Pamoja kuanzia tarehe 1 Julai 2010. Tarehe 1 Julai, 2010 itakumbukwa katika historia ya mtangamano wa Afrika Mashariki kama siku ambayo Jumuiya ya Afrika Mashariki ilianza rasmi utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja ambayo ni hatua ya pili na muhimu katika mtangamano wa Afrika Mashariki. Tofauti na Umoja wa Forodha ambao unalenga kuondoa vikwazo na kuruhusu uhuru wa biashara ya bidhaa miongoni mwa Nchi Wanachama, Soko la Pamoja linatoa uhuru na kuondoa vikwazo katika maeneo yote ya msingi katika uchumi wa Nchi Wanachama. Kwa kuzingatia unyeti wa hatua hii ya mtangamano, Nchi Wanachama zilikubaliana kuunda Soko la Pamoja hatua kwa hatua kulingana na ratiba ya utekelezaji iliyokubalika. Mfumo huu unalenga kuunda Soko la Pamoja imara, endelevu na lenye manufaa kwa Nchi zote Wanachama.

### 8.2.2.1 Maeneo ya msingi katika Soko la Pamoja

Soko la Pamoja la Afrika Mashariki linalenga kupanua na kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi na kijamii miongoni wa Nchi Wanachama kwa maslahi ya kila Nchi Mwanachama. Ushiriki wa Tanzania katika Soko la Pamoja la Afrika Mashariki unatarajiwa kuwa na manufaa yafuatayo:

a) Kuongezeka kwa uzalishaji na biashara kutokana na kuchochewa na fursa nyingi zaidi za kimasoko;
b) Kuwepo kwa uhuru wa ajira ndani ya Jumuiya kutawezesha Watanzania wengi kupata fursa za ajira na kuongeza ujuzi na uzoefu kutokana na maingiliano ya kijamii na kiuchumi;
c) Soko la Pamoja litachochea uwekezaji kwa vile litaambatana na uwekaji wa sera, sheria na taratibu zinazolenga kukuza na kuendeleza Sekta Binafsi.
d) Kuimarika kwa miundombinu ya kiuchumi na kijamii kutokana na utekelezaji wa miradi ya pamoja ya kikanda.

Kwa mujibu wa Ibara ndogo za 76(1) na 104(2) za Mkataba wa kuanzisha Jumuiya

### 8.2.4 Shirikisho la Kisiasa

Shirikisho la Kisiasa ni hatua ya nne katika mtangamano ambayo inategemea sana misingi imara itokanayo na utekelezaji wa hatua za mwanzo za mtangamano. Mwaka 2006 Nchi Wanachama zilikusanya maoni kutoka kwa wananchi juu ya kuharakisha au kutoharakisha uundwaji wa Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki. Matokeo ya mchakato huo yaliwasilishwa katika mkutano wa Wakuu wa Nchi Wanachama *(Summit)* uliofanyika Agosti 2007. Nchi za Uganda na Kenya ziliunga mkono uharakishaji wakati wananchi wa Tanzania walipinga hoja ya kuharakisha uanzishwaji wa Shirikisho la Kisiasa, na kuunga mkono utekelezaji wa mtangamano hatua kwa hatua. Asilimia 75.9 ya Watanzania walipinga uharakishwaji wa kuanzishwa Shirikisho la Kisiasa, wakati asilimia 64.9 ya wananchi wa Kenya waliunga mkono, na asilimia 56.3 ya wananchi wa Uganda waliounga mkono uharakishwaji wa Shirikisho la Kisiasa. Kwa kuwa Nchi za Rwanda na Burundi zilikuwa ngeni katika Jumuiya na hivyo hazikushiriki katika mchakato huo, Wakuu wa Nchi Wanachama waliziagiza kufanya mchakato huo. Nchi hizo zilikamilisha mchakato na kuwasilisha ripoti katika Mkutano wa 11 wa Wakuu wa Nchi uliofanyika Novemba, 2009. Nchi hizo mbili ziliunga mkono uharakishwaji wa uundwaji wa shirikisho la kisiasa.

Ili kuhakikisha kuwa mawazo ya wananchi, hususan wananchi wa Tanzania waliopinga uharakishwaji wa shirikisho la kisiasa yanazingatiwa, Wakuu wa Nchi Wanachama wameliagiza Baraza la Mawaziri la Jumuiya kuunda timu ya wataalamu kufanya uchambuzi wa kero na hofu zilizoainishwa na wananchi wakati wa mchakato wa kukusanya maoni na kutoa mapendekezo ya jinsi ya kukabiliana nazo. Kukubaliana kufanya uchambuzi wa kero, hofu na changamoto na kupendekeza jinsi ya kukubaliana nazo ni miongoni mwa mafanikio ya ushirikiano katika Jumuiya, kwani ni ishara ya dhamira ya kweli miongoni mwa Nchi Wanachama kuendeleza mtangamano na kwa kuwasikiliza wananchi wake.

### 8.2.5 Uimarishaji wa Sekta Binafsi

Katika miaka hamsini tangu Tanzania ipate uhuru, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki imechangia katika uendelezaji wa Sekta Binafsi kwa lengo kuiwezesha kutumia fursa zitokanazo na mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wizara imekuwa ikiandaa ziara za wafanyabiashara wa Tanzania kutembelea na kukutana na wafanyabiashara wa Afrika Mashariki na pia kuwashirikisha katika maonesho ya kibiashara ya Jua Kali/ Nguvu Kazi.

Lengo la ziara hizo ni kuwapa fursa wafanyabiashara kupata masoko ya bidhaa wanazozalisha katika Nchi Wanachama na kukutana na wafanyabiashara wa nchi hizo ili kukuza ushirikiano wa kibiashara miongoni mwao. Ziara hizo zimepata mafanikio ikiwa ni pamoja na kupata Soko la Bidahaa na fursa nyingine za kibiashara zilizopo katika Nchi za Afrika Mashariki. Aidha wafanyabiashara wameunda umoja wao wa kibiashara unaoitwa *Friends of East Africa*. Umoja huo una lengo la kubadilishana taarifa za kibiashara, uzoefu na mbinu za kufanya biashara katika soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

*Katika ziara hizo, Tanzania Private Sector Foundation (TPSF)* ikiwa mwakilishi wa vyama vya sekta binafsi nchini ilifanikiwa kusaini Hati za Makubaliano *(Memorandum of Understanding)* na vyama vya sekta binafsi vya nchi zilizotembelewa na ujumbe wa Tanzania. Makubaliano hayo yalilenga zaidi kuboresha ushirikiano katika shughuli mbalimbali za kuendeleza biashara na uwekezaji miongoni wa wanachama wao.

Wafanyabiashara wa Tanzania walipata fursa ya kukutana ana kwa ana na wafanyabiashara wa nchi zilizotembelewa na kufanikiwa kujenga uhusiano wa kibiashara; ambapo wanaendelea kuwasiliana na kufanya biashara. Wizara inaandaa utaratibu wa kupata mrejesho kutoka kwa wafanyabishara waliohudhuria ziara ili kupina mafanikio yanayopatikana kutokana na ziara hizo katika biashara na kubuni utaratibu wa kuboresha ziara hizo.

Aidha, Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki umeainisha kuwa sekta binafsi ni miongoni mwa mihimili mikuu ya kuendeleza ushirikiano katika Jumuiya. Kwa kuwa sekta binafsi bado ni changa, Nchi Wanachama zimejiwekea utaratibu wa kuandaa maonyesho ya kikanda ya sekta isiyo rasmi kila mwaka, maarufu kama Maonyesho ya Jua Kali/Nguvu Kazi. Madhumuni ya maonyesho haya ni kujenga sekta isiyo rasmi ili hatimaye ikue na kufikia ngazi ya sekta rasmi. Maonyesho ya Jua Kali/Nguvu Kazi yametoa fursa kwa wajasiriamali wa Tanzania kukutana na kubadilishana mawazo na uzoefu, na wafanyibiashara wenzao wa Nchi za Jumuiya juu ya kukuza na kuendeleza biashara zao, kujifunza teknolojia mpya na kuanzisha uhusiano wa kibiashara.

### 8.2.6 Ushirikiano baina ya Jumuiya (EAC) na Kanda nyingine

#### 8.2.6.1 Utatu wa EAC-COMESA-SADC *(EAC-COMESA-SADC Tripartite Arrangement)*

Katika jitihada za kupanua wigo wa kikanda, hususan, baina ya kanda za kiuchumi za Afrika Mashariki *(East African Community - EAC)*, Kusini mwa Afrika *(Southern Africa Development Community -SADC)* na Mashariki na Kati *(Common Market for Eastern and Southern Africa - COMESA)* Viongozi Wakuu wa Jumuiya hizo katika Mkutano wao wa tarehe 20 Oktoba, 2008 uliofanyika Kampala, Uganda walikubaliana kuanza mchakato wa kuanzisha Eneo Huru la Biashara, na hatimaye Umoja wa Forodha wa Nchi Wanachama za EAC-COMESA-SADC. Nchi Wanachama wa EAC-COMESA-SADC zinakamilisha maandalizi ya ratiba ya utekelezaji *(roadmap)* wa Eneo hilo Huru la Biashara, na mfumo wa kitasisi.

Kuundwa kwa Eneo huru la Kibiashara la Nchi Wanachama wa EAC-COMESA-SADC kutasaidia kupunguza gharama za kufanya biashara kwa kuwianisha taratibu za kiforodha, viwango vya ushuru wa forodha na kuondoa vikwazo vya kibiashara visivyo vya kiforodha (NTB). Aidha Utatu huu utaongeza soko la Bidhaa za Kilimo na Viwanda, ajira na kuinua kipato cha wananchi na pato la Taifa kwa ujumla. Soko la COMESA-EAC-SADC likajumuisha Nchi 26 mbazo ni: Angola, Botswana, Burundi, Comoros, Democratic Republic of Congo, Djibouti, Egypt, Eritrea, Ethiopia, Kenya, Libya, Lesotho, Madagascar, Malawi, Mauritius, Mozambique, Namibia, Rwanda, Seychelles, South Africa, Sudan, Swaziland, Tanzania, Uganda, Zambia, na Zimbabwe.

### 8.2.6.2 Ubia wa Kiuchumi kati ya Jumuiya ya Afrika Mashairiki na Jumuiya ya Ulaya

Katika miaka Hamsini ya Uhuru, Nchi Wanachama ikiwa ni pamoja na Tanzania, zimefanikiwa kuendeleza unafuu wa kodi uliyokuwa ukitolewa na Jumuiya ya Ulaya kupitia makubaliano mbalimbali ya ushirikiano wa kibiashara. Kwa sasa Nchi Wanachama zinaendelea na majadiliano ya Mkataba wa Ubia wa Kiuchumi *(Economic Partnership Agreement - EPA)* kati ya nchi za kundi la Afrika, Caribean na Pasifiki (ACP) na Jumuiya ya Ulaya (EC). Majadiliano yalianza mwaka 2002 ikiwa ni majadiliano ya jumla. Majadiliano haya yaliingia sehemu ya pili mwaka 2003 ambapo nchi za ACP zilijigawa kwenye makundi ambayo ziliona yanafaa.

Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuzingatia maagizo ya Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2002, zimefanikiwa kuendelea na majadiliano kama kundi moja katika majadiliano ya WTO na EU/ACP, kwa kuweka saini ya awali ya makubaliano (initialing) ya Mkataba wa Mpito wa Ubia wa Uchumi *(Framework for Economic Partnership Agreement – FEPA)* tarehe 27 Novemba 2007. Katika mkataba wa mpito nchi za EAC ziliainisha kufungua masoko yake kwa bidhaa za Jumuiya ya Ulaya kwa asilimia 82.6 kuanzia mwaka 2010 hadi 2032, na kuweka asilimia 17.4 kwenye orodha ya bidhaa nyeti. Jumuiya ya Ulaya kwa upande wake ilifungua soko lake kwa bidhaa kutoka nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa asilimia 100 *(Duty Free Quota Free – DFQF)*. Aidha mkataba huu wa mpito uliainisha katika ibara ya 37 maeneo ya kuendelea na majadiliano ili kufikia mkataba kamili.

Majadiliano ya Ubia wa Kiuchumi baina ya EAC na EC yameendelea na kukamilika katika maeneo mengi kama Ushuru wa Forodha, Viwango vya Afya ya Binadamu, Wanyama na Mimea, Vikwazo vya Kiufundi vya Biashara, Ushirikiano wa Forodha na Uwezeshaji wa Biashara. Aidha majadiliano yanaendelea katika maeneo yaliyosalia.

## 8.3 Mafanikio Katika Utekelezaji wa Miradi na Programu za Kikanda

### 8.3.1 Uendelezaji wa Miundombinu

Uendelezaji wa miundombinu ni miongoni mwa mafanikio ya miaka hamsini ya uhuru kutokana na ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kubuniwa mipango kabambe na mikakati ya uendelezaji miundombinu, hususan barabara, reli, usafirishaji na umeme. Jumuiya imebuni na inaendelea kutekeleza mipango kabambe ifuatavyo:

a) Mpango Kabambe wa kuendeleza Mtandao wa Barabara katika Jumuiya *(The East African Road Network Project)*;

b) Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Reli ya Afrika Mashariki *(The EAC Railways Development Masterplan)*;

c) Mpango Kabambe wa Upatikanaji wa Nishati ya Umeme katika Jumuiya *(EAC Power Master Plan)*; na

d) Usafirishaji wa Mawasiliano.

Maelezo mafupi na mafanikio ya utekelezaji wa miradi na mipango hii ni kama ilivyoainishwa katika aya zifuatazo:

### 8.3.2 Uendelezaji wa Barabara

Mpango Kabambe wa kuendeleza Mtandao wa Barabara katika Jumuiya *(The East African Road Network Project)* unaojumuisha kanda *(corridor)* tano. Kanda hizo ni:

**a.) Kanda ya Kwanza *(Corridor 1)*:**
Mombasa - Malaba - Katuna - Kigali-Kanyaru - Haut - Bujumbura-Gatumba ikijumuisha Marangu –Tarakea, Chalinze – Segera na Segera – Himo;

**b.) Kanda ya Pili *(Corridor 2)*:**
Dar-es-salaam-Isaka-Lusahunga-Mutukula-Masaka, na Lusahunga-Nyakasanza Rusumo-Kigali-Gisenyi;

**c.) Kanda ya Tatu *(Corridor 3)*:**
Biharamulo - Mwanza - Musoma - Sirari - Lodwar – Lokichogio ambayo pia ni sehemu
ya mtandao wa barabara katika ukanda wa Ziwa Victoria (Lake Victoria Road Circuit);

**d.) Kanda ya Nne *(Corridor 4)*:**
Tunduma - Sumbawanga - Kigoma – Manyovu (Mugina) – Rumonge – Bujumbura
– Ruhwa (Bugarama) – Karongi –Gisenyi; na

**e.) Kanda ya Tano *(Corridor 5)*:**
Tunduma - Iringa – Dodoma - Arusha - Namanga – Moyale.

Utekelezaji wa ujenzi wa mtandao wa barabara wa Jumuiya katika kanda hizo tano umefikia hatua mbali mbali kama ifuatavyo:

**Arusha – Namanga – Athi River**

Ujenzi wa barabara ya Arusha – Namanga – Arthi River yenye urefu wa Kilomita 104.4 kwa upande wa Tanzania na kilomita 136 upande wa Kenya unaendelea vizuri. Kasi ya ujenzi wa barabara hii iliongezeka ambapo hadi kufikia Desemba 2010, Kilometa 87 zilikuwa zimewekwa lami. Aidha, ujenzi ulifikia asilimia 63 ya kazi zote za ujenzi wa mradi.

**Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina (Feasibility Studies and Detailed Design) wa Barabara ya Arusha – Holili/Taveta - Voi**

Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Arusha – Holili – Voi yenye urefu wa kilomita 118 upande wa Tanzania unaendelea ambapo Mshauri Mwelekezi alianza kazi mwezi Septemba 2009 na anatarajiwa kumaliza kazi hiyo mwezi Aprili, 2011. Mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kilomita 110 upande wa Kenya yanaendelea sambamba na upande wa Tanzania.


**Barabara ya Malindi – Lunga Lunga na Tanga – Bagamoyo**

Kampuni ya M/s Aurecon ya Afrika Kusini ilisaini Mkataba wa kufanya kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara hii mapema Mwezi Desemba 2010. Kazi hii imeanza kutekelezwa mwezi Februari, 2011.

**Barabara ya Tanga – Horohoro**

Kufikia mwezi Desemba, 2010 Mkandarasi ameendelea na kazi ya ujenzi wa barabara hii yenye urefu wa kilomita 66 kutoka Horohoro mpaka wa Tanzania na Kenya hadi Tanga mjini ambayo imepata ufadhili kupitia mradi wa *Millenium Challenge Corporation* la Serikali ya Marekani. Ujenzi huo bado upo katika hatua za awali za uchimbaji na usawazishaji eneo la ujenzi ambapo kilomita 15 zimekamilika.

# Mtandao wa Barabara wa Afrika Mashariki




*Note*
*1 This map is not to scale It should therefore not be used for any other purpose other than purposes of reflecting the general alignment of the East African Road Network Corridors*

*2 The additional road links aer in dotted lines in colours similar to the Corridors of their alignment*

1 ———— Mombasa-Malaba-Katuna Corridor
2 ———— Dar-es-Salaam-Mwanza-Musoma-Siran-Lodwar-Lokichogio Corridor
3 ———— Biharamulo-Mwanza-Musoma-Sirari-Lodwar-Lokichogio Corridor
4 ———— Nyakanzi-Kasulu-Sumbwanga-Tunduma Corridor
5 Tunduma-Iringa-Dodoma-Arusha-Namanga-Moyale Corridor
6 ———— Sections/Links connecting with East Africa neighbours, those of interregional connectivity

### 8.3.3 Uendelezaji wa Reli Sekta ya Reli

Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekamilisha maandalizi ya Mpango kabambe wa Maendeleo ya Reli wa Afrika Mashariki *(The EAC Railways Development Masterplan)* uliodhinihwa mwaka 2009. Mtandao huu kwa upande wa Tanzania umeainisha njia zifuatazo:


a.) Liganga - Mchuchuma - Mtwara;
b.) Mchuchuma - Mbambabay;
c.) Liganga - Mlimba; Dar es Salaam - Mtwara;
d.) Isaka - Kigali - Kabanga;
e.) Keza – Ruvubu – Gitega – Musongati;
f.) Isaka - Kigali - Biharamulo - Bukoba - Masaka;
g.) Tunduma- Sumbawanga- Mpanda - Kigoma;
h.) Uvinza – Bujumbura;
i.) Mbegani (Bagamoyo)Port – Kidomole; na
j.) Tanga - Arusha – Musoma.

Katika kutekeleza Mpango Kabambe wa reli, majadiliano kuhusu kuunganisha reli kati ya Dar es Salaam na Isaka, na ujenzi wa reli ya Isaka-Kigali/Keza – Gitega – Musongati unaolenga kuziunganisha nchi za Tanzania, Rwanda, Burundi na DRC na kuendeleza matumizi ya Bandari ya Dar es Salaam yamekamilika. Aidha, kazi ya upembuzi yakinifu ilikamilika mwaka 2009 kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika iliogharimu kiasi cha Dola za Marekani 12 milioni.

Ujenzi wa reli hiyo yenye jumla ya Kilometa 1,651 unaokisiwa kugharimu Dola za Marekani bilioni 5.1, utahusisha ujenzi wa reli mpya na ya kisasa kuanzia Isaka-Kigali/Keza hadi Musongati yenye urefu wa Kilometa 681 na ujenzi wa reli kutoka Isaka hadi Dar es Salaam yenye urefu wa Kilometa 970. Reli ya Isaka- Kigali/Keza hadi Musongati inakisiwa kugharimu Dola za Marekani bilioni 2.63 na ujenzi wa reli kutoka Isaka hadi Dar es Salaam kupitia Bandari ya Bagamoyo utagharimu Dola za Marekani bilioni 2.47.

Aidha, Serikali za Tanzania na Uganda zimekubaliana kushirikiana kujenga reli ya Tanga – Arusha- Musoma – Port Bell/New Kampala. Hati ya makubaliano *(Memorandum of Understanding - MOU)* ya ushirikiano wa ujenzi wa reli hiyo kati ya Tanzania na Uganda umekamilika. Serikali hizi mbili zinashirikiana katika kutafuta fedha za kutekeleza mradi huu.

## Mitandao ya reli yaliyopo na yaliyopendekezwa Jumuiya ya Afrika Mashariki




**Legend**

| | |
|---|---|
| Current Railway Line | ——— |
| Proposed Railway Line | ——— |
| Ferry | - - - - - - - - |

### 8.3.4 Uendelezaji wa Sekta ya Nishati


Mpango kamambe wa upatikanaji wa Nishati ya Umeme katika Jumuiya *(EAC Power Master Plan)* unalenga kuimarisha uwezo wa Nchi wanachama kuzalisha na kusambaza umeme kwenye Kanda ya Afrika Mashariki.

Pamoja na mambo mengine, mpango huu nakusudia kuipatia umeme miji ya mipakani kupitia umeme unaozalishwa katika Nchi Wanachama *(crossborder electrification)*. Utekelezaji wa mpango huu umeanza kwa kuipatia umeme miji ya Lungalunga nchini Kenya kutoka mji wa Horohoro nchini Tanzania, na mji wa Namanga nchini Tanzania umepatiwa umeme kutoka mji wa Namanga (Kenya). Aidha, Mkoa wa Kagera unapata umeme kutoka Uganda na upembuzi yakinifu kwa ajili ya mradi wa kuupatia umeme mji wa Mutukula nchini Tanzania kutoka mji wa Mutukula nchini Uganda umekamilika.

Aidha, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki inaendelea na mazungumzo kati yake na Serikali ya Uganda kuhusu mradi wa kuzalisha umeme wa Murongo/Kikagati (mpakani mwa Uganda na Tanzania) kwa lengo la kuwezesha uwekezaji unaotarajiwa kuzalisha umeme wenye msongo wa 16MW. Mradi huu utakapokamika utawezesha kuipatia umeme miji ya Murongo na maeneo mengine Wilayani Karagwe.

Ili kukabiliana na upungufu wa nishati ya umeme, Nchi za EAC na SADC zimekubaliana kuanzisha mpango wa kuunganisha umeme ambao unalenga kuunganisha mifumo ya kitaifa ya umeme ujulikanao kwa jina la Southern Africa Power Pool. Kwa kuanzia mpango huu utaunganisha nchi za Zambia, Tanzania, na Kenya ambapo Tanzania itapokea umeme wenye msongo wa 400 KV kutoka mji wa Pensulo nchini Zambia. Umeme utapita katika miji ya Mbeya, Iringa, Dodoma, Singida, Arusha na hatimaye mji wa Nairobi nchini Kenya. Mradi huu ni wa miaka saba (2010/2011 – 2016/2017) ambapo Tanzania itachangia Dola za Marekani Milioni 309.1 kati ya Dola za Marekani Milioni 860 zinazohitajika kutekeleza mradi huu.

## Njia za umeme zilizopo na zijazo za Jumuiya ya Afrika Mashariki



### 8.3.5 Sekta ya Usafiri wa Anga

Nchi Wanachama zimeendelea kujipanga katika kuimarisha usafiri wa anga. Miongoni mwa mafanikio yaliypatikana ni kuanzishwa Wakala wa Usimamizi wa Usalama wa Anga katika Jumuiya *(East Africa Civil Aviation Safety and Security Oversight Agency - CASSOA)* ambao umeimarisha hali ya usalama wa usafiri wa anga hivyo kujenga misingi imara ya kuvutia uwekezaji katika sekta ya anga. Tangu kuanzishwa kwa chombo hiki mwaka 2007 masuala yafuatayo yametekelezwa:

d.) Uboreshaji wa usalama wa anga kulingana na viwango vilivyowekwa na Shirika la Kimataifa linalosimamia usafiri na usalama wa anga (ICAO);

e.) Kuandaa na kutumia Kanuni zilizowianishwa na Kanuni za usalama wa anga za Kimataifa *(East Africa Harmonized Safety and Security Aviation Regulations)* ambazo zinatambulika na ICAO;

a.) Kuanzishwa kwa mpango wa mafunzo ya pamoja ya marubani na waongoza ndege katika nchi wanachama ili kuendana na mabadiliko yanayotokea katika sekta ya usafiri wa anga duniani na hivyo kutoa leseni ya urubani ya Afrika Mashariki;

b.) Kupitia CASSOA Jumuiya imefanya utafiti unaolenga kubainisha mfumo wa kuratibu na kusimamia masuala ya usalama wa Anga ya Juu kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC Upper Flight Information Regional Project)*; na

c.) Kupitia CASSOA Jumuiya imeanzisha mfumo rahisi wa mawasiliano ya Anga *(Cheaper Navigation System)* utakaotumia mfumo wa *Global Navigation Satellite System (GNSS)*. Mfumo huu utapunguza gharama za mawasiliano ya anga.

Aidha, Nchi Wanachama zimeanzisha mpango kabambe wa miaka kumi wa kuendeleza viwanja vya ndege vilivyopewa kipaumbele katika Jumuiya ili viwe vituo vya Kimataifa na Kikanda vya kuingilia na kutokea kwenye vivutio vya utalii kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa mtandao wa utalii katika Jumuiya. Viwanja vya ndege vitakavyohusika katika mpango huu ni Arusha, Ziwa Manyara, Kigoma, Mafia, Kilwa Masoko na Loliondo.

### 8.3.6 Sekta ya Usafiri wa Majini

Ushirikiano wa kikanda katika Jumuiya ya Afika Mashariki umechangia katika uimarishaji wa usalama na uokoji wa wavuvi na wasafiri katika maeneo ya Maziwa. Katika eneo hili, Tanzania imenufaika kwa Makao Makuu ya Taasisi ya Uratibu wa Usalama na Uokozi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki *(Inland Waterways Maritime Search and Rescue Coordination Centre – MRCC)* kuwa mjini Mwanza.

### 8.3.7 Kuanzisha Vituo vya Pamoja vya Utoaji Huduma Mipakani *(One Stop Border Posts - OSBPs)*

Nchi Wanachama zimekubaliana kuanzisha vituo vya pamoja vya mipakani (One Stop Boarder Posts OSBP). Uanzishaji wa vituo hivi unalenga kurahisisha

taratibu za uhamiaji na forodha kwa kutoa huduma hizi upande mmoja wa mpaka bila kulazimika kupitia taratibu kama hizi upande wa pili wa mpaka. Hatua hii inawezesha biashara na usafirishaji shehena kufanyika kwa urahisi na gharama nafuu baina ya Nchi Wanachama.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Rwanda zimekubaliana kuanzisha Kituo cha Huduma za Pamoja Mpakani Rusumo (Billateral Agreement on Establishment of One Stop Border Post-Rusumo). Uanzishwaji wa kituo hicho unakwenda sambamba na ujenzi wa daraja la Rusumo ambalo ni kiungo muhimu kati ya Tanzania na Rwanda. Serikali ya Japan kwa kupitia Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan – JICA litagharamia ujenzi wa kituo na Daraja la Rusumo. Maandalizi ya uanzishwaji wa vituo vingine vya pamoja vya mpakani yanaendelea ili kuanzisha vituo Namanga, Horohoro/Lungalunga, Sirali/Isebania, Mutukula na Holili/Taveta.

### 8.3.8 Miradi ya Zanzibar

Mkakati wa Maendeleo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 2006 – 2010 unajumuisha miradi ifuatayo toka Tanzania Zanzibar:

a) Uwanja wa Ndege wa Karume;

b) Ujenzi wa Bandari ya Maruhubi; na

c) Ujenzi wa Cherezo *(Dry dock construction na Roll On –Roll Off (RORO)* kati ya Bandari za Zanzibar, Dar es Salaam na Mombasa.

Baraza la Mawaziri wa Kisekta ya Usafirishaji, Mawasiliano na Hali ya Hewa (TCM) limekwishaidhinisha miradi hii kuwa miongoni mwa miradi inayotafutiwa fedha katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Jumuiya inaendelea na majadiliano na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kuhusu ufadhili wa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Karume. Aidha, mradi wa Bandari ya Maruhubi ni miongoni mwa miradi ya kipaumbele katika Mikakati ya usafiri wa Jumuiya *(EAC Trasport Strategy)*. Mradi wa Ujenzi wa Cherezo (Dry dock construction na Roll on – Roll Off (RORO) kati ya Bandari za Zanzibar, Dar es Salaam na Mombasa ni miongoni mwa vipaumbele katika Ushirikiano wa Utatu wa Kikanda *(Tripartite COMESA-EAC-SADC)*.

### 8.3.9 Uendelezaji wa Sekta ya Kilimo

Katika kuhimiza maendeleo ya Sekta ya Kilimo kwa lengo la kukuza biashara ya bidhaa za Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Tanzania ilifanikiwa kuzishawishi nchi nyingine wanachama kuiweka sekta ya kilimo katika vipaumbele vya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tayari Nchi Wanachama zimeandaa Mpango Maalum wa Kilimo na Usalama wa Chakula.

Aidha majadiliano ya uanzishaji wa Itifaki ya Afya ya Wanyama na Mimea *(SPS Protocol)* ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yanaendelea vizuri. Itifaki hiyo itakapokamilika itawezesha kuhuisha viwango na kurahisisha biashara miongoni

Nchi Wanachama zimekubaliana kutekeleza Mpango wa Jumuiya wa Kulinda na Kuimarisha Haki za Binadamu katika Jumuiya.

Mafanikio mengine yaliyopatikana ni Nchi Wanachama kusaini Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Uratibu wa Sera za Nje *(EAC Foreign Policy Coordination)* ambayo ipo katika hatua za kuridhiwa na Nchi Wanachama. Aidha, majadiliano kwa ajili ya Itifaki ya Hadhi na Kinga za Kibalozi *(EAC Protocol in Immunities and Privileges)* yanaendelea.

**8.3.11.4 Utawala Bora na Haki za Binadamu**

Katika kuimarisha demokrasia miongoni mwa Nchi Wanachama, Jumuiya inaendeleza demokrasia miongoni mwa Nchi Wanachama. Katika kuhakikisha utawala bora unazingatiwa, Wakuu wa vyombo vya kupambana na rushwa hukutana mara kwa mara kwa lengo la kubadilishana uzoefu na kuwa na mikakati ya pamoja. Aidha, Nchi Wanachama zimekamilisha majadiliano ya uundwaji wa Itifaki ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Ili kuhakikisha haki za binadamu zinalindwa na kuzingatiwa Jumuiya inaratibu vikao vya wakuu wa Tume za Haki za Binadamu kutoka Nchi Wanachama na kwa pamoja wamekubaliana kutekeleza mpango wa kulinda na kuimarisha haki za binadamu katika Jumuiya.

Vilevile, Itifaki ya Jumuiya ya Uratibu wa Sera za Nje *(EAC Foreign Policy Coordination)* imesainiwa na Wakuu wa Nchi sasa ipo kati hatua za kuridhiwa na Nchi Wanachama. Aidha, majadiliano kwa ajili Itifaki ya Hadhi na Kinga za Kibalozi *(EAC Protocol in Immunities and Privileges)* yanaendelea.

**8.3.12 Utekelezaji wa Mradi wa Utunzaji wa Mazingira na Matumizi Endelevu ya Ziwa Victoria (LVEMP II)**

Kumekuwepo na mafanikio katika utunzaji wa mazingira na matumizi endelevu ya raslimali kikanda, hususan kupitia katika Mradi wa Utunzaji na Usimamizi wa Mazingira katika Bonde la Ziwa Victoria, (Lake Victoria Environment Management Programme – LEVEMP) na Sera ya Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi *(EAC Climate Change Policy)*.

Awamu ya Kwanza ya Mradi huo ilitekelezwa katika Nchi za Kenya, Uganda na Tanzania kwa Kipindi cha Mwaka 1997 hadi 2005, kwa kufanya utafiti kwa lengo la kubaini hali halisi ya uharibifu wa mazingira na hali ya maisha ya jamii inayozunguka Ziwa Victoria ili kuweza kuandaa Mpango Kamambe wa Utunzaji na Usimamizi wa Mazingira katika Bonde la Ziwa Victoria.

Matokeo ya utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya Mradi ambayo yalikuwa ni katika utafiti yalioonyesha kuwa kuna uharibifu mkubwa katika Ziwa Victoria ambao unahitaji kudhibitiwa. Uharibifu huo ulikuwa ni pamoja na ongezeko la magugu maji na uharibifu wa baionuwai yakiwemo maeneo oevu *(Wetlands)* ambapo udhibiti ulihitajika kupitia utekelezaji wa mradi wa muda mrefu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali hususan jamii inayolizunguka Ziwa Victoria.

Kutokana na matokeo ya utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya Mradi, Jumuiya

ya Afrika Mashariki inatekeleza Awamu ya Pili ya Mradi huu (LVEMP II) ambayo ina vipengele vikuu vinne ambavyo ni:

a.) Kuimarisha mfumo wa Utendaji kwa kujenga uwezo wa usimamizi wa Programu *(Strengthening Institutional capacity for managing the program)*;
b.) Mpango wa Kuthibiti uchafuzi wa udongo;
c.) Uratibu wa Mpango wa Usimamizi wa maji *(water shed)*;
d.) Uhifadhi na Usimamizi wa vyanzo vya maji na kuboresha maisha ya Jamii inayolizunguka eneo la Mradi.

Utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mradi wa Utunzaji na Usimamizi wa Mazingira katika Bonde la Ziwa Victoria (LVEMP II) ulianza Mwezi Agosti, 2009 na utakamilika Mwaka 2013. Makao Makuu ya Mradi huu yako Mkoani Mwanza. Kwa Tanzania miji ya Geita, Nansio na Sengerema itanufaika kupitia vipengele vya mradi huo, ambavyo ni pamoja na:

a.) Kuthibiti uchafuzi wa udongo;
b.) Mpango wa Usimamizi wa maji *(water shed)*;
c.) Uhifadhi na usimamizi wa vyanzo vya maji na kuboresha maisha ya jamii inayolizunguka eneo la mradi.

### 8.3.13 Ujenzi wa Makao Makuu ya Jumuiya

Arusha imekuwa Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki tangu mwaka 1967. Kwa sasa makao makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yapo katika jengo la Makao Makuu ya Jumuiya iliyovunjika, lililojengwa miaka ya 1970, jengo ambalo kwa sasa linamilikiwa na Tanzania kufuatia mgawanyo wa mali za iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Jengo hilo ni Kituo cha Mikutano ya Kimataifa *(Arusha International Conference Centre- AICC)*. Uamuzi wa kuendelea kuwa na Jumuiya, mara Sekretariet ya Tume ya Kudumu ya Utatu ilipoanzishwa mwaka 1996, ulifuatiwa na wazo la kujenga Makao Makuu ya Jumuiya. Ujenzi huo haukuweza kuanza mara moja kutokana na Sekretariet hiyo kutokuwa na ardhi ya kujenga Makao Makuu hayo na kukosekana kwa fedha za ujenzi huo.

Kutokana na kupanuka kwa shughuli za Jumuiya, Nchi Wanachama zilikubaliana kujenga Jengo la kisasa linalokidhi mahitaji ya sasa na ya baadaye kadiri Mtangamano unavyokuwa. Mchakato wa ujenzi wa Makao Makuu ulianza mara baada ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoa ekari 9.85 za ujenzi wa Makao Makuu mwaka 2001. Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ilianza kutafuta fedha za ujenzi wa Makao Makuu hayo. Serikali ya Shirikisho la Ujerumani ilikubali kutekeleza Mradi huo kwa kutoa Euro 8 milioni. Gharama za ujenzi ziliongezeka kutokana na kupanuka kwa mahitaji hasa baada ya nchi ya Burundi na Rwanda kujiunga na Jumuiya, hadi kufikia Euro 14 milioni. Serikali ya Shirikisho la Ujerumani ilikubali kuongeza kiasi kilichopungua cha Euro 6 milioni.

Ujenzi ulianza kwa Wakuu wa Nchi Wanachama kuweka jiwe la msingi tarehe 20 Novemba 2009. Ujenzi huu unaofadhiliwa na Serikali ya Ujerumani kwa gharama

Soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki kukuza biashara, uwekezaji, viwanda, kilimo, na kujiletea maendeleo kiuchumi na kijamii.

Ushirikiano wa kikanda ikiwemo Jumuiya ya Afrika Mashariki ni mwanzo tu wa ushirikiano mpana na wa kina utakaoziunganisha Jumuiya za maendeleo za kikanda barani Afrika na kuzaa Jumuiya kubwa zaidi ya Afrika.

Kwa hiyo, matarajio ya Wizara katika kipindi cha miaka 50 ijayo ni kuona juhudi za sasa za Tanzania zinazoendelea kisera, kimikakati za kukabiliana na mfumo wa biashara na uchumi wa dunia zinakuwa kichecheo cha kukuza uwekezaji, uzalishaji, tija na kuwezesha Tanzania kujenga uchumi imara na mahiri na kunufaika na fursa za kikanda na kimataifa na maendeleo ya watanzania. Kwa kutumia ushirikiano wa kikanda Tanzania itajiimarisha kiuchumi na kuligeuza taifa kuwa miongoni mwa nchi zilizoendelea duniani. Kama hatua za mwanzo, inatarajiwa Tanzania itaweza kuitumia fursa ya kipekee ya kujiografia (kama nchi inayopakana na nchi 10) kuwa lango na kitovu cha biashara katika Afrika ya Mashariki, Afrika ya kati na kusini mwa Afrika.

Uendelezaji wa miundombinu kitaifa na kikanda utawezesha Tanzania kuendeleza bandari, barabara, reli viwanja vya ndege katika viwango vinavyokubalika kimataifa na hivyo kuwa lango kuu na kitovu cha biashara. Tanzania inapakana na nchi za Msumbiji, Malawi, Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Burundi, Rwanda, Uganda na Kenya.

Mwelekeo wa kuwa na Jumuiya iliyopanuka zaidi si wa kufikirika, kwani tayari Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, SADC, COMESA wanaendelea na maandalizi ya kuanzisha ushirikiano baina ya kanda hizi tatu (COMESA-EAC-SADC Tiripartite Arrangement). Hivyo upo uwezekano mkubwa katika miaka hamsini ijayo Nchi za Afrika kujiunga na kuwa na Jumuiya ya Afrika ambayo itaunganisha Jumuiya ndogo ndogo za kikanda zilizopo sasa Afrika. Bara la Afrika litakuwa limejigeuza kuwa Jumuiya moja kubwa ya kiuchumi inayolingana na mabara mengine ikiwemo Jumuiya ya Ulaya. Kwa maana hiyo, Jumuiya ndogo kama Afrika Mashariki zitatoweka, kwanza kwa kuziunganisha Jumuiya za EAC, SADC na COMESA na kisha Jumuiya zote barani Afrika kuunganishwa na kuunda Jumuiya moja kwa bara lote la Afrika itakayokuwa na Soko la Pamoja na Sarafu Moja.

**IMETOLEWA NA WIZARA YA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI JULAI, 2011**

## Kiambatanisho Na.6:
## MIRADI ILIYOONGOZA KATIKA UWEKEZAJI KUTOKA NCHI ZA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (IDADI, THAMANI KATIKA DOLA ZA KIMAREKANI, NA AJIRA)

| **UZALISHAJI** | | | |
|---|---|---|---|
| **MWAKA** | **MIRADI** | **THAMANI** | **AJIRA** |
| 2005 | 5 | 8 01 | 127 |
| 2006 | 12 | 15 07 | 2,163 |
| 2007 | 15 | 7 64 | 255 |
| 2008 | 23 | 231 22 | 429 |
| 2009 | 21 | 30 70 | 1,143 |
| 2010 | 10 | 16 55 | 1,761 |
| **JUMLA** | **86** | **395.19** | **5,878** |
| **UJENZI** | | | |
| **MWAKA** | **MIRADI** | **THAMANI** | **AJIRA** |
| 2005 | 3 | 3 06 | 17 |
| 2006 | 9 | 7 85 | 53 |
| 2007 | 4 | 2 78 | 21 |
| 2008 | 13 | 19 16 | 67 |
| 2009 | 3 | 3 83 | 29 |
| 2010 | 11 | 17 34 | 395 |
| **JUMLA** | **43** | **54.02** | **582** |
| **KILIMO** | | | |
| **MWAKA** | **MIRADI** | **THAMANI** | **AJIRA** |
| 2005 | 1 | 3 25 | 107 |
| 2006 | 1 | 6 67 | 206 |
| 2007 | 2 | 7 82 | 1524 |
| 2008 | 3 | 9 28 | 12 |
| 2009 | 2 | 0 65 | 21 |
| 2010 | 3 | 11 90 | 1,382 |
| **JUMLA** | **12** | **39.57** | **3,252** |
| **USAFIRISHAJI** | | | |
| **MWAKA** | **MIRADI** | **THAMANI** | **AJIRA** |
| 2005 | 2 | 2 34 | 87 |
| 2006 | 3 | 4 62 | 363 |
| 2007 | 4 | 2 16 | 106 |
| 2008 | 9 | 11 20 | 226 |
| 2009 | 3 | 8 07 | 141 |
| 2010 | 4 | 23 72 | 722 |
| **JUMLA** | **25** | **52.11** | **1,645** |
| **UTALII** | | | |
| **MWAKA** | **MIRADI** | **THAMANI** | **AJIRA** |
| 2005 | 3 | 2 30 | 40 |
| 2006 | 5 | 2 71 | 213 |
| 2007 | 4 | 2 82 | 29 |
| 2008 | 11 | 11 56 | 164 |
| 2009 | 5 | 3 98 | 181 |
| 2010 | 3 | 1 96 | 68 |
| **JUMLA** | **31** | **25.33** | **695** |

## KIAMBATANISHO A: MAENEO YALIYOFUNGULIWA KATIKA SOKO LA PAMOJA

### I. Uhuru wa raia wa Afrika Mashariki kufanya kazi katika Nchi yoyote ndani ya Jumuiya (Free Movement of Workers)

Kada zitakazohusishwa na ufunguaji wa soko la ajira ambazo zimefunguliwa kwa raia toka Nchi Wanachama ni kama ifuatavyo:

### A. TANZANIA

(i) Walimu wa vyuo vya elimu ya juu na vyuo vikuu wenye shahada ya uzamivu kuanzia 2010;
(ii) Walimu wa shule za sekondari katika fani ya hisabati, fizikia, bailojia kuanzia 2011)
(iii) Walimu wa shule za sekondari katika fani ya lugha za kigeni kuanzia 2015;
(iv) Walimu wa shule za msingi zinazofundisha kwa lugha ya kiingereza wenye angalau shahada ya kwanza kuanzia 2010 isipokuwa kwa upande wa Tanzania Visiwani;
(v) Walimu wa vyuo vya Kilimo, Ufundi Stadi wenye kiwango cha elimu cha angalau shahada ya pili katika fani husika kuanzia (2010);
(vi) Wahandisi wa madini kuanzia 2011;
(vii) Wahandisi wa majengo kuanzia na wahandisi wengine 2012;
(viii) Maafisa ugani katika sekta ya kilimo kuanzia 2015;
(ix) Wauguzi na wakunga kuanzia 2010;
(x) Wahudumu wengine wa sekta ya afya kuanzia 2015;
(xi) Kada ya waongoza ndege kuanzia 2012; na
(xii) Kada ya upimaji ramani kuanzia 2015.

### B. KENYA

(i) Wakurugenzi na watendaji wakuu wa makampuni (2010);
(ii) Wakuu wa vyuo Vikuu na taasisi nyingine za elimu (2010);
(iii) Mameneja wa makampuni (2010);
(iv) Wanasayansi na wahandisi (2010);
(v) Wataalam wa hisabati, takwimu na kopyuta (2010);
(vi) Madaktari, wauguzi na wakunga (2010);
(vii) Walimu wa sekondari na vyuo (2010);
(viii) Wanasheria (2010);
(ix) Wahasibu (2010);
(x) Wataalam wa Makataba, watunzi, wasanii (2010); na
(xi) Madaktari wa wanyama (2010).

### C. UGANDA

(i) Mameneja wa makampuni (2010);
(ii) Wakuu wa vyuo vikuu na taasisi nyingine za elimu (2010);
(iii) Wataalam wa Kompyuta (2010);

(iv) Wasanii (2010);
(v) Mafundi mchundo, mafundi magari na umeme (2010);
(vi) Wanasheria (2010);
(vii) Wataalam wa anga na marubani (2010);
(viii) Wahandisi wa ujenzi na umeme (2010).

## D. RWANDA

(i) Wataalam katika fani ya sayansi (2010);
(ii) Wataalam wa hisabati, takwimu na utafiti (2010);
(iii) Wataalam wa afya (2010);
(iv) Wataalam wa Bailojia, mimea, wanyama na mazingira (20100;
(v) Wahandisi wa ujenzi, wasanifu majengo na mipango miji (2010);
(vi) Walimu wa Sekondari na vyuo vya ufundi (2010);
(vii) Walimu wa elimu maalum (vipofu, viziwi, mtindio wa ubongo), (2010);
(viii) Wahandisi (2010);
(ix) Mafundi sanifu (2010);
(x) Wataalam wa Kompyuta, utafiti na mipango (2010)

## E. BURUNDI

(i) Wataalam wa Sayansi (hesabu, fizikia, wahandisi wa sayansi, kemia, takwimu, kopyuta, wasanifu majengo na wahandisi (2010);
(ii) Wataalam wa afya, madaktari, wauguzi na wakunga (2010);
(iii) Wataalam wa Kopyuta (2010);
(iv) Wahandisi (2010);
(v) Mafundi sanifu (2010);
(vi) Wataalam wa Biashara, maktaba, sayansi jamii, waandishi wa vitabu, wabunifu na wasanii (2010);
(vii) Wahubiri wa dini (2010).

Kada nyingine zitaendelea kufunguliwa hatua kwa hatua kwa kuzingatia mahitaji na utayari wa Nchi wanachama.

## II: Uhuru wa kufanya Biashara ya Huduma katika Nchi Yoyote Ndani ya Jumuiya (Free Movement of Services)

Kwa kuanzia Nchi wanachama zimekubaliana kuondoa vikwazo katika sekta saba za huduma zilizoanishwa katika jedwali la uhuru wa biashara ya huduma kama ifuatavyo:

(viii) Sekta ya Huduma za Biashara
(ix) Sekta ya Huduma za Mawasiliano;
(x) Sekta ya Huduma za Ugavi;
(xi) Sekta ya Huduma za Elimu;

(xii) Sekta ya Huduma za Fedha;
(xiii) Sekta ya Huduma za Utalii;
(xiv) Sekta ya Huduma za Usafiri

Mchanganuo wa sekta na aina za huduma zilizokubalika kufunguliwa na Nchi Wanachama na vipindi vya kuanza utekelezaji ni kama ifuatavyo:

## A. TANZANIA

### SEKTA YA HUDUMA ZA BIASHARA (Business Services)

**(i) Huduma za Utaalam (Professional Services)**

a) Biashara ya Huduma za Uhasibu na Ukaguzi (2010)
b) Biashara ya Huduma ya Uhandisi (2010)
c) Biashara ya Huduma ya Ukunga na Wahudumu wa Hospitali (2011)
d) Biashara ya Huduma ya Utabibu na Huduma za Meno (2010)

**(ii) Huduma za ukodishaji na upangishaji**

Biashara ya huduma za kukodisha Meli, Ndege, na Mitambo ya kisasa ya Usafirishaji (2010)

**(iii) Huduma nyingine za Kibiashara**

a) Biashara ya huduma za utafiti wa masoko na ukusanyaji wa kura za maoni *(Market Research an Public Opinion Polling Services)* (2010)
b) Biashara ya huduma ya ajira ya watumishi *(Placement and Supply Services of Personnel)* (2010)

### SEKTA YA HUDUMA ZA UGAVI (Distribution Services)

**(i) Huduma ya Uwakala (2010)**
**(ii) Huduma ya Haki Maalum ya Uendeshaji (Franchising)**

### SEKTA YA HUDUMA ZA ELIMU (Education Services)

(i)Huduma za Elimu ya Msingi (2010)
(ii) Huduma za Elimu ya Sekondari (2010)
(iii) Huduma Nyingine za Elimu

a) Biashara ya Huduma za Elimu ya Ufundi (2010)
b) Biashara ya Huduma za Elimu ya Chuo Kikuu (2010)
c) Biashara ya Huduma za Elimu ya Watu Wazima (2010)

### SEKTA YA HUDUMA ZA USAFIRI (Transport Services)

(i) Huduma za Usafiri wa Anga (2015)
(ii) Huduma za Usafiri wa Majini (2010)

(ii) Huduma za Elimu ya Sekondari (2010)
(iii) Huduma za Elimu ya Juu (2010)
(iv) Huduma za Elimu ya watu wazima (2010)
(v) Huduma nyingine za Elimu (2010)

**SEKTA YA HUDUMA ZA BENKI NA FEDHA (2010)**
(i) Huduma za Benki na Fedha (2010)
(ii) Huduma za Bima (2010)

**SEKTA YA HUDUMA ZA UTALII**
(i) Huduma za Hoteli na Migahawa (2010)
(ii) Huduma za Uwakala wa Usafiri na Uongozaji Watalii (2013)
(iii) Huduma za Uongozaji Watalii (2015)

**SEKTA YA HUDUMA ZA USAFIRI**
(i) Huduma za Usafiri wa Majini (2012)
(ii) Huduma za Usafiri wa Anga (2010)
(iii) Huduma za Usafiri wa Reli (2010)
(iv) Huduma za Usafiri wa Barabara (2010)
(v) Huduma za Usafiri kwa njia ya Bomba (2010)
Sekta nyingine zitaendelea kufunguliwa hatua kwa hatua kwa kuzingatia mahitaji na utayari wa Nchi wanachama.

III: Uhuru wa raia wa Afrika Mashariki kuwekeza mitaji katika Nchi yoyote ndani ya Jumuiya *(Free movement of Capital)*

Vikwazo katika soko la mitaji la Tanzania na ratiba ya kuviondoa ni kama ifuatvyo:
(i) Raia wa kigeni hawaruhusiwi kununua zaidi ya asilimia 60 ya hisa katika soko la mitaji kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kikwazo hiki kinatarajiwa kuondolewa ifikapo mwaka 2015. Kwa upande wa Jamhuri ya Kenya, Jamhuri ya Uganda na Jamhuri ya Rwanda hakuna kikwazo hiki;
(ii) Kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania raia wa kigeni hawaruhusiwi kushiriki katika soko la amana na hati fungani sa Serikali; kikwazo hiki kinatarajiwa kuondolewa ifikapo 2012. Nchi nyingine Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki hazina kikwazo hiki;
(iii) Raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hawaruhusiwi kukopesha nje ya nchi ambapo kikwazo hiki kinatarajiwa kuondolewa ifikapo 2015; na
(iv) Raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hawakuruhusiwa kuwekeza nje ya nchi ambapo kikwazo hiki kinatarjiwa kuondolewa ifikapo 2014.

TRADE
MARK